# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2026 NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2026/2027

## KITABU CHA PILI

**TUME YA MIPANGO - ZANZIBAR**

**JUNI, 2026**

## YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................1
2.0 MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2026...............2
2.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia...............................................................2
2.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika ..............................................................4
2.3 Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.........................................................................................4
2.4 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika ya Mashariki .......................................5
2.5 Mwelekeo wa Mfumuko wa Bei wa Dunia ............................................7
3.0 MWELEKEO WA UCHUMI WA ZANZIBAR 2026 .............................8
5.0 MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2026/2027 ...........................................................................12
6.0 MIRADI YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2026/2027.......................12
7.0 RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/2026 ..................................14
8.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO KWA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO NA SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2026/2027..................................... 16
8.1 Afisi ya Rais Ikulu.....................................................................................16
8.2 Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ......................17
8.2.1 Mahkama Kuu.........................................................................................19
8.3 Afisi ya Rais-Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ...........................................................................................19
8.3.1 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ...........................25
8.3.2 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)...............................26
8.5.2 Kikosi cha Valantia. ...........................................................................27
8.5.3 Chuo cha Mafunzo .................................................................................27
8.5.4 Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ..........................................................28
8.5.5 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi .........................................................29
8.4 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ................................................30

8.4.1 Mamlaka ya Usimamzi wa Mazingira ........ 33
8.4.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya ........ 34
8.5 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi ........ 35
8.6 Wizara ya Afya ........ 36
8.6.1 Hospitali ya Mnazi Mmoja ........ 43
8.7 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ........ 44
8.8 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ........ 45
8.9 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ........ 46
8.10 Wizara ya Fedha na Mipango ........ 50
8.10.1 Tume ya Mipango Zanzibar ........ 54
8.10.2 Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ........ 57
8.11 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ........ 60
8.12 Wizara ya Kazi na Uwekezaji ........ 61
8.13 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ........ 62
8.14 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ........ 68
8.15 Wizara ya Maji, Nishati na Madini ........ 71
8.16 Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu ........ 83
8.17 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ........ 83
8.18 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ........ 90
8.19 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ........ 96
8.20 Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji ........ 99
8.21 Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar ........ 99
9.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI ........ 101
10.0 WASHIRIKA WA MAENDELEO ........ 101
11.0 HITIMISHO ........ 102

## 1.0 UTANGULIZI

Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027 ni hatua ya mwanzo ya utekelezaji wa mipango ya muda wa kati katika kipindi cha pili cha Awamu ya Nane ya uongozi wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kupitia utekelezaji wa mpango huu, Serikali inalenga kuongeza kasi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi pamoja na kuimarisha misingi ya uchumi endelevu na utawala bora. Uzingatiaji wa malengo ya mipango ya muda wa kati na muda mrefu ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na maelekezo mbali mbali ya Serikali kwa Wizara na Taasisi katika uandaaji wa Mpango huu utaimarisha uwajibikaji, usimamizi bora wa rasilimali na utekelezaji wenye tija wa shughuli za maendeleo nchini.

kwa mwaka wa 2026, uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa asilimia 7.5 kutokana na Serikali kuendelea kuchukua juhudi za kuimarisha sekta ya utalii, kudhibiti mfumuko wa bei, uhamasishaji katika ukusanyaji wa mapato, uimarishaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji pamoja na kuendelea na utekelezaji miradi mikubwa ya maendeleo. Miradi hiyo itahusisha sekta za ujenzi, uzalishaji, utalii pamoja na utoaji wa huduma muhimu za kijamii ikiwemo afya, elimu, maji, umeme na usalama wa nchi na wananchi. Vile vile, Serikali itaendelea kuweka mazingira bora yatakayowezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na kuchangia ukuaji wa uchumi wa Zanzibar.

Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027, utaelekeza nguvu katika utekelezaji wa programu na miradi inayolenga kukuza uchumi jumuishi, kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za jamii, kuongeza mapato ya Serikali, kupanua fursa za ajira, pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na wananchi. Lengo kuu ni kufanikisha matokeo ya haraka na yenye tija katika maendeleo ya Taifa, sambamba na kuinua ustawi wa wananchi kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na ujumuishwaji wa makundi yote ya kijamii.

Kitabu hiki kinaelezea Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2026 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027 kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo yaliyobainishwa katika mipango ya muda wa kati ya kitaifa. Vile vile, kiimezingatia malengo na mikakati ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 (SDGs), Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050, Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050 pamoja na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063. Hivyo, utekelezaji wa Mpango huu unatarajiwa kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kufikia maendeleo endelevu na ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

## 2.0 MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI

### 2.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), ya mwezi wa April 2026, uchumi wa dunia umetikisika na unatarajiwa kufikia kiwango cha wastani wa ukuaji wa asilimia 3.1 mwaka 2026, ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 mwaka 2025. Ukuaji huu mdogo unatokana na kuzuka kwa vita vya Mashariki ya kati (Marekani-Israili dhidi ya Irani) ambavyo vitapelekea kupanda kwa bei za bidhaa za mafuta, kupanda mfumko wa bei pamoja na masharti magumu ya kifedha Duniani. Aidha, kupungua kwa kasi ya ukuaji uchumi wa Nchi Zilizoendelea hasa kwa Mataifa makubwa kama vile Japan ambayo kwa mwaka 2026 uchumi wake unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 0.7 kutoka wastani wa asilimia 1.2 mwaka 2025, Canada kufikia asilimia 1.5 mwaka 2026 kutoka wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2025 pamoja na nchi nyengine za Umoja wa Ulaya zinazotarajiwa kupungua kufikia wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2026 kutoka wastani wa 3.0 mwaka 2025.

**Kwa Nchi Zilizoendelea,** kasi ya ukuaji wa uchumi inatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 1.8 mwaka 2026 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.9 mwaka 2025. Uchumi wa nchi za Umoja wa Ulaya unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 1.1 mwaka 2026 kutoka ukuaji wa asilimia1.4 mwaka 2025. Hali hii inatokana na kuongezeka kwa ugumu wa sera za kifedha hususan ongezeko

la viwango vya riba katika nchi nyingi zilizoendelea kwa lengo la kudhibiti mfumko wa bei, kupungua kwa upatikanaji wa mikopo, uwekezaji na uzalishaji hasa katika sekta ya viwanda na ujenzi. Aidha, uwepo wa migogoro ya kisiasa za Kijiografia (Geopolitics) na kiusalama hususan vita kati ya Marekani na Israili dhidi ya Irani, ambavyo vinaathiri ukanda wa Mashariki ya Kati na kuathiri mtiririko wa biashara ya kimataifa, kwa kuongezeka bei za nishati, gharama za usafirishaji na upatikanaji wa bidhaa muhimu katika masoko ya dunia.

**Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi,** unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2026 ukilinganishwa na wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2025. Kuongezeka kwa mvutano wa kisiasa kati ya Marekani na Israili dhidi ya Irani kunachangia kuleta athari hasi kwa uchumi wa Nchi Zinazoendelea kwa kupanda kwa bei za nishati na kuvurugika kwa minyororo ya usambazaji hususan kwa nchi zinazoagiza nishati kutoka nje. China ni moja ya nchi ambayo inaongoza katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi hizi, mwaka 2026 uchumi wa China unatarajiwa kukua kwa asilimia 4.4 kutoka asilimia 5.0 mwaka 2025.

Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa China, kama mdau mkubwa wa biashara na uwekezaji kwa nchi nyingi zinazoendelea, kunatarajiwa kuwa na athari za moja kwa moja katika biashara ya kimataifa na bei za bidhaa. Kupungua kwa mahitaji ya China kunaweza kushusha bei za malighafi na bidhaa za msingi katika soko la dunia, hali itakayopunguza mapato ya nchi zinazotegemea mauzo ya bidhaa hizo na hivyo kudhoofisha mizani ya biashara katika kipindi kifupi. Kwa kuzingatia uhusiano wa karibu uliopo kati ya uchumi wa Nchi Zinazoendelea na mwenendo wa uchumi wa Dunia pamoja na Nchi Zilizoendelea, kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi hizo inatarajiwa kupungua kutokana na kudorora kwa mahitaji ya kimataifa. Hali hii inatarajiwa kupunguza uhitaji wa bidhaa na huduma kutoka nchi zinazoendelea na kudhoofisha mauzo ya nje, mapato ya fedha za kigeni na shughuli za uzalishaji katika sekta mbalimbali.

## 2.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Bara la Afrika

Uchumi wa Bara la Afrika unatarajiwa kukua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2026, sawa na ukuaji kama huo wa mwaka 2025. Ukuaji huu unatokana na ongezeko la uwekezaji katika miundombinu, nishati na sekta za huduma, pamoja na kuendelea kuimarika kwa matumizi ya ndani katika baadhi ya nchi. Aidha, kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta na gesi katika nchi kama Nigeria, Angola, Libya na Algeria, pamoja na kuanza kwa uzalishaji mpya katika nchi ya Senegal na Mozambique, kunatarajiwa kuongeza mchango wa sekta ya nishati katika ukuaji wa bara la Afrika. Katika ngazi ya nchi, ukuaji wa juu unatarajiwa kwenye baadhi ya nchi kama Uganda, Guinea, Benin na Rwanda, ambazo zinatarajiwa kufikia ukuaji wa zaidi ya asilimia 6.0 kutokana na uwekezaji katika miundombinu, viwanda, kilimo cha kisasa na kuimarika kwa mahitaji ya ndani.

Licha ya matarajio ya kuongezeka wa ukuaji wa uchumi wa Afrika mwaka 2026, kasi hiyo bado iko chini ya kiwango kinachohitajika kufikia maendeleo jumuishi na endelevu. Hivyo, nchi za Afrika zinahitaji kuimarisha mageuzi ya kimuundo, kuongeza thamani ya uzalishaji, kuimarisha biashara ya kikanda kupitia utekelezaji wa "African Continental Free Trade Area", na kuwekeza katika rasilimali watu na teknolojia ili kuongeza ushindani na ustahimilivu wa uchumi dhidi ya mishtuko ya nje.

## 2.3 Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara

Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (Sub-Saharan Afrika) unatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2026 ukilinganisha na wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2025. Upungufu huu mdogo unatokana na kupanda kwa bei za nishati na chakula, madeni makubwa ambayo huathiri uwekezaji na biashara pamoja na kupungua kwa usafirishaji wa mauzo ya malighafi katika Ukanda huu kutokana na mabadiliko ya bei za bidhaa

duniani. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi katika baadhi ya nchi kama vile Niger, Sychells, Namibia, Togo, Zimbabwe na Senegal imepungua. Kwa upande wa nchi ya Senegal kasi ya ukuaji uchumi inatarajiwa kupungua na kufikia asilimia 2.2 mwaka 2026 kutoka wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2025. Upungufu huu unatokana na kukamilika kwa hatua ya awali ya miradi mikubwa ya mafuta na gesi na kuingia hatua ya kawaida ya uzalishaji pamoja na mabadiliko ya bei za mafuta ambayo huathiri mapato ya nchi na kwa upande wa Seychells kasi ya ukuaji inatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 1.5 mwaka 2026 kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2025. Hii imesababishwa na kupungua kwa mapato ya utalii kutokana na mwenendo wa hali ya uchumi duniani na mvutano wa kijiografia.

Hata hivyo, nchi kama vile Nigeria kasi ya ukuaji Uchumi inatarajiwa kukua na kufikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2026 ukilinganisha na wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2025, Guinea unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2026 ukilinganisha na wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2025. Hii inatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hasa madini ya 'bauxite' na 'iron ore', kuongezeka kwa miradi mikubwa ya uwekezaji kama vile miradi ya migodi, miundombinu na usafirishaji ambayo huongeza ajira na uzalishaji kwa kiwango kikubwa. Aidha, nchi ya Ethiopia kasi ya ukuaji uchumi inatarajiwa kufikia asilimia 9.2 mwaka 2026 sawa na ukuaji kama huo kwa mwaka 2025.

Mwelekeo wa uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara unaonesha uwepo wa fursa za kuimarika endapo nchi zitaendelea kutekeleza mageuzi ya kimuundo, kuboresha mazingira ya biashara, na kuwekeza katika sekta zenye tija kubwa ili kuongeza ushindani na ustahimilivu wa uchumi dhidi ya changamoto za migogoro ya vita baina ya Marekani- Israil na Iran inayoendelea.

## 2.4 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika ya Mashariki

Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2026 unatarajiwa kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 5.7 sawa na ukuaji kama

huo kwa mwaka 2025. Ongezeko hilo linatokana na kupungua kwa vikwazo vya biashara na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa kati ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji wa ndani na sekta binafsi kwenye viwanda na biashara.

Kwa kuangalia mwenendo wa uchumi kwa Nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka 2026, Uchumi wa **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, umefikia wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2026 sawa na ukuaji kama huo mwaka 2025. Hii ni kutokana na Serikali kudumisha utulivu wa mfumuko wa bei, kuongezeka kwa uzalishaji wa dhahabu, madini mengine pamoja na maandalizi ya gesi asilia. Nchi ya **Kenya**, kasi ya ukuaji wa uchumi inatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2026 kutoka asilimia 4.9 mwaka 2025. Hii inatokana na mapato mengi hutumika kulipia madeni ya Serikali na kupelekea kupunguza uwezo wa Serikali kuwekeza kwenye miradi mipya ya Serikali, kupanda kwa bei za mafuta duniani ambayo huathiri mfumuko wa bei na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na uagiziaji kutoka nje. Kwa upande wa **Burundi** kasi ya ukuaji wa uchumi inatarajiwa kufikia wastani wa asilimi 3.8 mwaka 2026 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2025. Hii ni kutokana na kupungua kwa uwekezaji wa sekta binafsi na miundombinu, mabadiliko ya tabianchi ambayo huathiri uzalishaji pamoja na kutokuwa na mashirikiano mazuri na nchi wanachama wa kibiashara.

Hata hivyo, baadhi ya nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki uchumi wake unaendelea kuimarika. Uchumi wa **Uganda** unatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 7.5 kwa mwaka 2026 kutoka wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2025. Hii ni kutokana na kuimarika kwa sekta ya kilimo kama vile kilimo cha kahawa, chai pamoja na pamba ambayo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa hilo. Aidha, kuwepo kwa miradi mikubwa ya uzalishaji wa mafuta na gesi ambayo itapelekea kuongezeka kwa ajira na fedha za kigeni. Nchi ya Rwanda kasi ya ukuaji uchumi unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 7.2 kwa mwaka 2026 kutoka asilimia 7.0 mwaka 2025, ukuaji huu utatokana na

kuengezeka kwa uwekezaji katika sekta binafsi na uchumi wa kidijitali, kuwepo kwa sera nzuri za kiuchumi na utulivu wa mfumuko wa bei na kuwepo kwa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Mageuzi ya Kiuchumi, na nchi ya **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo** kasi ya ukuaji uchumi inatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2026 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2025. Ukuaji huu unatokana na kuongezeka kwa uzalishaji na mauzo ya madini muhimu kama cobalt na shaba (copper), licha ya changamoto za miundombinu, usalama na utawala.

### 2.5 Mwelekeo wa Mfumuko wa Bei wa Dunia

Kasi ya mfumuko wa bei duniani inatarajiwa kuongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2026 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2025. Kuongezeka kwa kasi ya mfumuko wa bei duniani kunatokana na kupanda kwa ushuru wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nchi Washirika wa Biashara duniani pamoja na uharibifu wa miundombinu muhimu ya nishati kumepelekea kuongezeka kwa bei za nishati na chakula.

Kwa upande wa **Nchi za Umoja wa Ulaya** kasi ya mfumuko wa bei inatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2026 kutoka wastani wa asilimia 2.1 mwaka 2025. Nchi Zilizoendelea kasi ya mfumuko wa bei inatarajiwa kuongezeka na kufikia wastani wa asilimia 2.8 kwa mwaka 2026 kutoka wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2025 na kwa **Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi** mfumuko wa bei unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2026 kutoka wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2025.

## 3.0 MWELEKEO WA UCHUMI WA ZANZIBAR 2026

Uchumi wa Zanzibar mwaka 2026 unatarajiwa kuimarika zaidi, sekta zinazotarajiwa kukua kwa kasi kubwa zaidi ni pamoja na sekta ya miundombinu, biashara, uwekezaji, sekta za huduma na viwanda.

### Malengo na Shabaha za Uchumi Jumuishi kwa Mwaka 2026

Mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2026 unakwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050, Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati (ZADEP) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030. Kwa takwimu za awali, uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa asilimia 7.5 mwaka 2026 kutoka ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2025 kutokana na sababu zifuatazo:

i Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Zanzibar kwa asilimia 9.3 kutoka watalii 917,167 kwa mwaka 2025 hadi watalii 1,002,917 mwaka 2026 kutokana na kuongeza masoko mapya ya utalii;

ii Kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo Miundombinu ya Barabara za Mjini na Vijijini, Ujenzi wa Uwanja wa Ndege - Pemba, Ujenzi wa Mji wa Serikali, Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani na Mpigaduri na Ujenzi wa Mji wa Michezo - Fumba. Miradi mengine itakayochangia ukuaji wa uchumi ni ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ikiwemo miundombinu ya afya, elimu, maji safi na salama, umeme na ujenzi wa viwanja vya michezo kwa kila Wilaya;

iii Kuendelea na hatua za kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ili kubakia kwa tarakimu moja;

iv Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuongeza thamani na miradi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi;

v Kuongezeka kwa mchango wa sekta binafsi kutokana na juhudi za Serikali za kukuza uwekezaji, uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira;

vi Kuongezeka kwa uhamasishaji wa ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa matumizi ya Serikali; na

vii Kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta ya uchumi wa buluu pamoja na kuimarisha matumizi endelevu ya bahari.

**Shabaha za Uchumi Jumla ni kama ifuatavyo:**

i. Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.5 mwaka 2026;
ii. Mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja chini ya kiwango cha asilimia 5 kama ilivyo shabaha iliyowekwa kwa nchi za Afrika Mashariki;
iii. Uwiano wa mapato ya ndani kufikia asilimia 41 ya Pato la Taifa mwaka 2026 kutoka asilimia 33.4 mwaka 2025;
iv. Uwiano wa mapato ya kodi kufikia asilimia 36 ya Pato la Taifa mwaka 2026 kutoka asilimia 33 mwaka 2025;
v. Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0;
vi. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi minne; na
vii. Kipato cha mwananchi kuendelea kubakia juu ya wastani wa Dola za Kimarekani 1,449.

**Matarajio ya Ukuaji huo yanategemea misingi ifuatayo:**

i. Kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa sera za kifedha;
ii. Kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya mafuta na gesi ili kuweza kupunguza gharama za bei za nishati hizo;
iii. Kuendelea kuimarika kwa miundombinu na huduma za bandari zetu ambazo zitapunguza gharama za upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu;
iv. Kuwa na uwekezaji zaidi katika sekta ya viwanda ili kuongeza thamani ya bidhaa kwa matumizi ya ndani na usafirishaji nje ya nchi;
v. Kuanza kwa miradi inayotarajiwa kuwa ni nyenzo za kuwezesha Zanzibar kukaribisha timu kwa mazoezi na baadhi ya mechi za mashindano ya mpira wa miguu kuwania Kombe la Afrika (AFCON 2027); na
vi. Kuendelea kuwepo kwa hali ya usalama nchini na kwa nchi jirani.

Aidha, Serikali inataendelea kuchukua hatua za kuweka utulivu wa bei kwa wananchi ikiwemo: -

i. Kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi;
ii. Kuendelea kutekeleza Sera ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania ili kutunza thamani ya Shilingi ya Tanzania na kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei;
iii. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Serikali itaendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani;
iv. Kuendelea kushajihisha na kuimarisha shughuli za uzalishaji viwandani;
v. Kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini; na
vi. Kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku hasa kwa vyakula vikuu vinavyolimwa hapa nchini.

Hata hivyo, makadirio ya kasi ya ukuaji wa uchumi yanaweza kuwa chini ya wastani wa asilimia 7.5 ikiwa mgogoro wa vita baina Marekani-Israili dhidi ya Irani utaendelea kudumu kwa muda mrefu na kupelekea kuathiri baadhi ya shughuli kuu za uchumi zikiwemo sekta ya utalii, usafirishaji, uwekezaji na biashara sambamba na kupanda kwa bei za mafuta ambazo zitaathiri uzalishaji wa ndani na uchumi wa Zanzibar ifikapo mwishoni mwa mwaka 2026.

Kufuatia mwenendo wa sasa wa uchumi wa dunia, hatua madhubuti za sera zinazopendekezwa ili kudhibiti athari hizo na kuimarisha uhimilivu wa uchumi wa Zanzibar mwaka 2026 zinajikita katika maeneo yafuatayo:

i. Sera za Fedha na Bajeti: Serikali inapaswa kulenga matumizi yenye tija kubwa, hususan katika miundombinu muhimu, afya, nishati na uzalishaji. Aidha, kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani bila kuongeza mzigo mkubwa kwa walipa kodi, pamoja na kuboresha usimamizi wa matumizi ya umma, kutasaidia kudhibiti nakisi ya bajeti na kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali;

ii. Sera za Fedha na Uthabiti wa Kifedha: Kupitia Benki Kuu ya Tanzania, juhudi zielekezwe katika kudhibiti mfumuko wa bei ili ubaki katika tarakimu moja, kusimamia ukwasi (liquidity) kwa uangalifu na kulinda uthabiti wa sekta ya fedha. Hatua hizi zitasaidia kupunguza athari za mfumuko wa bei za bidhaa kutoka nje, hususan nishati na chakula. Serikali inapaswa kuimarisha usimamizi wa bei za bidhaa muhimu na kuanzisha akiba ya kimkakati ya chakula na nishati ili kukabiliana na athari za mtikisiko wa uchumi wa dunia, kupunguza utegemezi na matumizi ya fedha za kigeni katika miamala ya ndani na kuimarisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa za msingi. Vilevile, kupunguza utegemezi wa uagizaji na hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya bei za bidhaa kutoka nje ya nchi katika uchumi wa Zanzibar.

iii. Usimamizi wa Sekta ya Nje: Kuimarisha mapato ya fedha za kigeni kupitia sekta ya utalii, mauzo ya bidhaa nje ya nchi ikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, mazao ya baharini na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI). Pia, juhudi za kubadili vyanzo vya nishati na kuongeza matumizi ya nishati mbadala zitasaidia kupunguza utegemezi wa mafuta kutoka nje na hivyo kupunguza athari za mabadiliko ya bei za bidhaa hiyo;

iv. Kuimarisha Sekta za Uzalishaji wa Ndani: Kuwekeza zaidi katika kilimo, uvuvi, viwanda vidogo na vya kati (SMEs), kuongeza thamani ya bidhaa (value addition) pamoja na kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Hatua hizi zitapunguza utegemezi wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kuongeza ajira pamoja na mapato ya ndani;

v. Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji: Kuendelea kurahisisha taratibu za uwekezaji, kupunguza urasimu na kuimarisha miundombinu ya biashara na huduma. Hii itasaidia kuvutia wawekezaji zaidi na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi ambayo ni msingi muhimu wa Uchumi; na

vi. Kuimarisha Mifumo ya Hifadhi ya Jamii: Kusimamia mifumo ya kusaidia kaya zilizo katika mazingira magumu dhidi ya athari za mfumuko wa bei, hususan kwa bidhaa muhimu za chakula. Hii itasaidia kulinda ustawi wa wananchi na kudumisha utulivu wa kijamii na kiuchumi.

Kwa ujumla, utekelezaji madhubuti wa sera hizi utawezesha Zanzibar kupunguza athari za mishtuko ya nje (external shocks), kuimarisha uthabiti wa uchumi, na kulinda matarajio ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2026 licha ya changamoto za kimataifa zinazoendelea.

## 4.0 MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2026/2027

Kwa mwaka 2026/2027, Mpango wa Maendeleo utaelekeza nguvu katika utekelezaji wa programu na miradi inayolenga kukuza uchumi jumuishi, kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za jamii, kuongeza mapato ya Serikali, kupanua fursa za ajira, pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na wananchi. Lengo kuu ni kufanikisha matokeo ya haraka na yenye tija katika maendeleo ya Taifa, sambamba na kuinua ustawi wa wananchi kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na ujumuishwaji wa makundi yote ya kijamii. Vipaumbele vitajikita katika kukamilisha miradi ya kimkakati, hususan ile inayohusiana na maandalizi ya Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027, kwa kuzingatia viwango vya kimataifa na ufanisi unaotakiwa. Aidha, Serikali itaendelea kukamilisha miradi iliyoanzishwa katika miaka iliyopita ili kuhakikisha inaleta matokeo yaliyokusudiwa na kuongeza thamani katika uchumi.

Utekelezaji wa Mpango huu utaongozwa na misingi ya utawala bora, uwajibikaji na uwazi, pamoja na matumizi yenye tija ya rasilimali za umma (value for money). Vile vile, mifumo ya ufuatiliaji na tathmini itaendelea kuimarishwa ili kuhakikisha utekelezaji unafanyika kwa ufanisi na malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa kwa wakati.

### 4.1 Miradi ya Kimkakati kwa Mwaka 2026/2027

Katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027, Serikali imedhamiria kutekeleza miradi maalum ya kimkakati katika maeneo mahsusi manne ambayo ni: **(i) Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi; (ii) Kuimarisha Miundombinu Wezeshi; (iii) Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii; na (iv)**

**Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu**. Lengo ni kuimarisha ukuzaji wa uchumi jumuishi, miundombinu itakayosaidia upatikanaji na ubora wa huduma za jamii na utawala bora. Kwa kuzingatia maeneo hayo, programu na miradi ya kimkakati inayotarajiwa kutekelezwa ni ifuatayo:

(i) **Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi:** Programu na miradi itakayotekelezwa katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

a) Programu ya Kuimarisha Bandari;
b) Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia;
c) Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Utalii;
d) Mradi wa Ujenzi wa Masoko;
e) Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya Kuchakata Samaki;
f) Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki;
g) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Uimarishaji wa Zao la Mwani;
h) Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula;
i) Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (TFSRP); na
j) Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa.

**(ii) Kuimarisha Miundombinu Wezeshi:** Programu na miradi itakayotekelezwa katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

a) Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu na za Ndani;
b) Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini;
c) Programu ya Ujenzi wa Barabara zinazoingia katika Mji wa Michezo Fumba;
d) Program ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar;
e) Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege;
f) Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar; na
g) Mradi wa Uwekaji wa Taa kwa Barabara ambazo hazina Taa za Barabarani Mjini na Vijijini.

**(iii) Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii:** Programu na miradi itakayotekelezwa katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

a) Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu;
b) Mradi wa Ujenzi wa Mji wa Michezo – Fumba;
c) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi;
d) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja;
e) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia ya Binguni; na
f) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali za Mikoa.

(iv) **Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu:** Programu na miradi itakayotekelezwa katika eneo hili ni kama ifuatavyo:

a) Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Kijeshi cha Kisasa cha Idara Maalum za SMZ;
b) Mradi wa Ujenzi wa Mji wa Serikali; na
c) Mradi wa Uboreshaji wa Mahkama.

## 4.2 Rasilimali kwa Ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2026/2027

Kwa mwaka 2026/2027, jumla ya TZS 5,779.15 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa programu 38 na miradi 54 ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho, TZS 4,433.80 bilioni, sawa na asilimia 76.72 ya bajeti ya maendeleo, zinatokana na mapato ya ndani. Aidha, TZS 1,345.35 bilioni, sawa na asilimia 23.28, zinatarajiwa kupatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ambapo TZS 240.10 bilioni ni ruzuku na TZS 1,105.25 bilioni ni mikopo. Muhtasari fedha zilizopangwa kwa utekelezaji wa programu na miradi ya maenendeleo kutoka Serikalini na Washirika wa Maendeleo kwa Maeneo Makuu manne ya Kimkakati unaonekana katika **Jadweli Nambari 1**.

**Jadweli nambari 1: Muhtasari wa Mgao wa Fedha Zilizopangwa kwa Upande wa Serikali na Washirika wa Maendeleo kwa Programu na Miradi kwa Maeneo Makuu kwa Mwaka 2026/2027**

| ENEO | MAKISIO KWA MWAKA 2026/2027 (TZS "000") | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **SMZ** | **%** | **RUZUKU** | **MKOPO** | **JUMLA YA FEDHA ZA WASHIRIKA WA MAENDELEO** | **%** | **JUMLA YA BAJETI YOTE** | **%** |
| **ENEO 1:** Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi | 678,132,391 | 79 | 81,644,643 | 99,924,480 | 181,569,123 | 21 | 859,701,514 | 15 |
| **ENEO 2:** Kukuza Uwezo wa Watu na Huduma za Jamii | 974,090,184 | 68 | 134,691,176 | 320,662,953 | 455,354,129 | 32 | 1,429,444,313 | 25 |
| **ENEO 3:** Kuimarisha Miundombinu Wezeshi | 1,556,976,319 | 71 | 9,003,720 | 631,515,122 | 640,518,842 | 29 | 2,197,495,161 | 38 |
| **ENEO 4:** Kuimarisha Utawala na Uhimilivu | 1,224,599,633 | 95 | 14,765,796 | 53,148,339 | 67,914,135 | 5 | 1,292,513,768 | 22 |
| **JUMLA KUU** | **4,433,798,527** | **77** | **240,105,335** | **1,105,250,894** | **1,345,356,229** | **23** | **5,779,154,756** | **100** |

## 5.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO KWA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO NA SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2026/2027

### 5.1 Afisi ya Rais Ikulu

Afisi ya Rais Ikulu inajukumu la kusimamia na kuratibu kwa ufanisi shughuli za Kiongozi Mkuu wa Nchi na kuhakikisha kuwa utekelezaji wa majukumu ya Serikali unazingatia Katiba ya Zanzibar pamoja na sheria na taratibu zilizowekwa. Afisi hii inawajibu wa kuimarisha uratibu wa maamuzi na maelekezo yanayotolewa na Baraza la Mapinduzi, ili kuhakikisha utekelezaji wake unakuwa wenye tija, uwazi na ufanisi katika maendeleo ya Zanzibar. Aidha, Afisi ya Rais Ikulu ina jukumu la kuendeleza na kuimarisha ushirikiano wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi (Diaspora), kwa lengo la kuwashirikisha kikamilifu katika maendeleo ya Taifa kupitia uwekezaji, uhamishaji wa maarifa na ushirikiano wa kiuchumi na kijamii.

Kwa mwaka 2026/2027, Afisi ya Rais Ikulu imepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo wenye thamani ya TZS 7.00 bilioni, kutoka Serikalini.

***Mradi wa Uimarishaji wa Majengo ya Ikulu***

Mradi una lengo la kuboresha na kuendeleza miundombinu ya majengo ya Ikulu ili yawe salama, yanayokidhi mahitaji ya kiutendaji ya Afisi ya Rais. Mradi huu utahusisha ukarabati na ujenzi wa sehemu muhimu za majengo, uboreshaji wa mifumo ya umeme, maji na TEHAMA, pamoja na kuimarisha viwango vya usalama na mazingira ya kazi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 7.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza na ujenzi wa Afisi na nyumba katika eneo la Afisi za Ikulu – Bwefum;
ii. Ukarabati wa miundombinu ya majengo ya Ikulu;

iii. Kuimarisha Afisi ya Usalama Serikalini; na
iv. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA na mawasiliano ya Ikulu.

## 5.2 Afisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

Afisi inadhamana ya kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na miongozo inayohusiana na masuala ya utawala bora Zanzibar ili kuhakikisha uwajibikaji, uwazi na usimamizi bora wa rasilimali za umma kwa manufaa ya wananchi. Afisi hii ina jukumu la kuhakikisha uwepo wa utumishi wa umma wenye ufanisi, unaozingatia viwango vya juu vya utendaji na utoaji wa huduma bora kwa jamii kwa kuzingatia misingi ya haki, sheria na demokrasia, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma zinazozingatia haki za binadamu kwa misingi ya usawa. Kwa mwaka 2026/2027, Afisi imepanga kutekeleza miradi mitatu (3) ya maendeleo kwa jumla ya gharama ya TZS 5.05 bilioni, kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Mradi wa Upatikanaji wa Haki za Kisheria***

Mradi unalengo la kuwawezesha wananchi kupata haki kwa wakati na kwa usawa, pamoja na kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wote kupitia mifumo thabiti ya kisheria. Kwa mwaka 2026/2027, Mradi umepagiwa kiasi cha TZS 1.72 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha mifumo ya kisheria pamoja na kuongeza uwezo wa Taasisi za sheria na rasilimali watu;
ii. Kuziwezesha Asasi za Kiraia kutoa msaada wa kisheria na kuhamasisha jamii kuhusu haki za kisheria na za kibinadamu, hususan kwa makundi hatarishi; na
iii. Kuanzisha na kuimarisha utaratibu wa uelimishaji kwa jamii kuhusu huduma za haki na za kisheria.

***Mradi wa Utoaji wa Huduma ya Haki kwa Kuzingatia Jinsia***

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wanawake na wasichana kwa kuwawezesha kupata huduma za kisheria katika kukabiliana na kesi za udhalilishaji na ukatili wa kijinsia. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 147.50 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha mazingira wezeshi yatakayochochea kuimarika kwa mfumo wa kisheria na kisera katika kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto; na
ii. Kuimarisha uwezo wa uratibu wa sekta mbalimbali katika kuzuia na kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

***Mradi wa Kujenga Msingi Imara wa Mapambano Dhidi ya Rushwa Tanzania***

Mradi huu una lengo la kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu madhara ya rushwa pamoja na kukuza ushirikiano kati ya Taasisi za umma, Sekta binafsi, na jamii katika kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 3.18 bilioni kutoka kwa Washrika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha usimamizi na ubora wa taarifa zinazowasilishwa kwa wachunguzi wa masuala ya rushwa;
ii. Kuimarisha mfumo wa haki jinai kwa kulinda haki za watuhumiwa, waathirika na mashahidi;
iii. Kuimarisha uongozi na uwajibikaji wa taasisi mbalimbali katika usimamizi wa taarifa za kiutawala; na
iv. Kuongeza uwezo wa mfumo wa haki jinai katika utambuzi, ufuatiliaji na usimamizi wa mali kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

### 5.2.1 Mahkama Kuu

Afisi hii ina jukumu la kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi katika mashauri ya jinai na madai yanayowasilishwa mahkamani, kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa usawa nchini. Kwa mwaka 2026/2027, Afisi imepanga kutekeleza mradi mmoja (1) wa maendeleo wenye thamani ya TZS 36.60 bilioni, (TZS 1.60 bilioni kutoka Serikalini na TZS 35.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Mradi wa Uboreshaji wa Mahkama***

Mradi huu una lengo la kuimarisha mifumo na miundombinu ya Mahkama ili kuwezesha upatikanaji wa haki pamoja na kuongeza tija na ufanisi kwa watendaji wa Mahkama nchini. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 36.60 bilioni, (TZS 1.60 bilioni zitatokana na Serikali na TZS 35.00 bilioni zitatokana na Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Ununuzi wa samani kwa ajili ya majengo ya Mahkama;
ii. Ununuzi wa vifaa saidizi vya TEHAMA; na
iii. Ununuzi wa huduma za kimtandao.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Ujenzi wa majengo ya Mahkama za Wilaya katika maeneo ya Kijichi, Makunduchi, Chwaka, Kinduni na Kigunda;
ii. Ukarabati wa majengo ya Mahkama ya Mahonda na Wete; na
iii. Kujenga uwezo kwa watumishi kuhusu usimamizi na utekelezaji wa miradi.

## 5.3 Afisi ya Rais - Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Afisi ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kuendeleza utawala bora katika Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na kutoa huduma za kiutawala kwa Idara

Maalum. Aidha, Afisi inahakikisha uwepo wa ufanisi, uwajibikaji, uwazi na ushirikishwaji wa wananchi katika mifumo ya utawala, kwa lengo la kuimarisha maendeleo endelevu, kudumisha utulivu na kuboresha utoaji wa huduma za umma kwa viwango vya kitaifa na kimataifa. Kwa mwaka 2026/2027, Afisi imepanga kutekeleza miradi tisa (9) ya maendeleo yenye jumla ya thamani ya TZS 358.03 bilioni, (TZS 350.18 bilioni kutoka Serikalini na TZS 7.86 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Mradi wa Ujenzi wa Masoko***

Mradi huu una lengo la kuimarisha na kuboresha miundombinu ya masoko nchini, ili kuwezesha wafanyabiashara na wajasiriamali kufanya shughuli zao katika mazingira bora, salama na yenye tija pamoja na wananchi kupata huduma. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuchochea ukuaji wa biashara, ajira, kuongeza kipato cha wananchi na kuimarisha uchumi wa ngazi ya jamii. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 65.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Ujenzi wa soko la Kibandamaiti na Kinyasini.

***Mradi wa Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri katika Soko la Mwanakwerekwe***

Mradi huu utahusisha ujenzi wa kituo cha kisasa na maegesho ya vyombo vya usafiri yatakayozingatia miundombinu imara, salama na endelevu katika soka la Mwanakwerekwe. Utekelezaji wa mradi huu unalenga kuongeza ufanisi wa huduma za usafirishaji, kupunguza msongamano wa magari pamoja na kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Aidha, mradi unatarajiwa kuboresha mazingira ya biashara na huduma kwa watumiaji wa soko, kwa kuimarisha urahisi wa upatikanaji wa huduma na usalama. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2026/2027 umepangiwa jumla ya TZS 47.00 bilioni.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza na ujenzi wa kituo na maegesho ya vyombo vya moto.

***Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Kisasa cha Kijeshi cha Idara Maalum za SMZ – (Awamu ya Kwanza)***

Mradi huu una lengo la kuimarisha na kuendeleza uwezo wa mafunzo ya kijeshi na kiusalama kwa watendaji wa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kuwezesha upatikanaji wa mafunzo ya kitaalamu na ya vitendo yanayokidhi viwango vya kimataifa. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kiusalama, kuimarisha taaluma na weledi wa watumishi, pamoja na kuchochea fursa za ajira kupitia maendeleo ya sekta ya mafunzo ya kijeshi na ulinzi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2026/2027 umepangiwa jumla ya TZS 70.00 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa majengo ya utawala pamoja na miundombinu ya msingi ya Chuo cha Kijeshi -Kikungwi;
ii. Ujenzi wa madarasa, vyumba vya majaribio (simulation) na viwanja vya mafunzo ya kijeshi na michezo;
iii. Ujenzi wa kituo cha afya na maeneo ya chakula kwa walimu na wanafunzi;
iv. Ujenzi wa mabweni ya askari wanafunzi na maafisa, pamoja na nyumba za walimu; na
v. Ujenzi wa bohari ya vifaa vya kijeshi, barabara za ndani na bustani za chuo.

***Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za afya za kibingwa kwa maafisa na wapiganaji, kwa lengo la kupunguza rufaa zisizo za lazima na kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma za afya ndani ya Idara Maalum. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuongeza ufanisi, kupunguza

gharama za rufaa na kuimarisha ustawi wa watumishi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka wa fedha 2026/2027 umepangiwa jumla ya TZS 30.00 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa hospitali ya rufaa ya Idara Maalum za SMZ- Kama;
ii. Ununuzi wa vifaa tiba na vifaa saidizi kwa ajili ya hospitali ya Rufaa ya Idara Maalum;
iii. Uandaaji wa mfumo wa taarifa za hospitali (Hospital Management Information System); na
iv. Ununuzi wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya na rufaa za dharura.

***Mradi wa Kuimarisha Haki Jinai***

Mradi unatarajia kujenga Chuo cha mafunzo cha kisasa katika eneo la Hanyegwa Mchana kwa lengo la kubadilisha tabia za watoto na vijana kwa kuwapa msaada unaohitajika kupitia chuo hicho ili kubadilisha tabia zao na kuweza kurejea katika jamii wakiwa raia wema na kuweza kushiriki katika shughuli za uzalishaji. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2026/2027, umepangiwa kiasi cha TZS 40.00 bilioni.

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa***

- Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Kurekebisha Tabia cha Hanyegwa Mchana.

***Mradi wa Ujenzi wa Afisi za Masheha Zanzibar***

Mradi una lengo la kuratibu shughuli mbalimbali za Serikali na kijamii kama vile usajili wa vizazi na vifo, uidhinishaji wa nyaraka na utoaji wa taarifa muhimu wa wananchi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2026/2027, umepangiwa kiasi cha TZS 40.00 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa Afisi za Masheha kwa Shehia 276 Unguja na Pemba; na
ii. Ununuzi wa samani za Afisi za Masheha kwa Shehia 276.

***Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama***

Mradi huu una lengo la kuimarisha usalama wa jamii kwa kuhakikisha uwepo wa miundombinu ya kisasa ya ulinzi na usalama, ikijumuisha uwekaji wa mifumo na vifaa vya kisasa vya ulinzi. Hatua hii inalenga kulinda wananchi na mali zao dhidi ya uhalifu pamoja na kupunguza viashiria hatarishi vya kiusalama katika jamii. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2026/2027 umepangiwa jumla ya TZS 40.18 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa vituo vya kamera za ufuatiliaji wa matukio katika maeneo ya Maisara - Unguja na Chake Chake, Wete na Mkoani - Pemba;
ii. Matengenezo, uboreshaji na uendeshaji wa mfumo wa kamera za ulinzi (CCTV) pamoja na vifaa vya mawasiliano vya ulinzi na usalama; na
iii. Ununuzi wa sare na vyombo vya usafiri kwa ajili ya Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

***Mradi wa Usafi na Upendezeshaji wa Miji***

Mradi huu una lengo la kuimarisha mazingira bora ya Miji kwa kuhakikisha usimamizi imara wa taka ngumu na majitaka, kuongeza na kuendeleza maeneo ya kijani, pamoja na kuboresha mandhari ya Miji ili iwe safi, salama na yenye kuvutia kwa wakaazi na wageni. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuchangia katika kuboresha afya ya jamii, kuimarisha uhimilivu wa Miji na kuongeza mvuto wa kiuchumi na kijamii wa maeneo ya mbalimbali ya Miji. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2026/2027 umepangiwa jumla ya TZS 18.00 bilioni.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Usafishaji wa barabara katika Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na matengenezo ya alama za barabarani;
ii. Ukusanyaji na uondoshaji wa taka ngumu kutoka maeneo ya makaazi na biashara;
iii. Uanzishaji, uendelezaji na uhifadhi wa bustani za barabarani pamoja na maeneo ya wazi; na
iv. Upendezeshaji na uboreshaji wa mandhari ya miji ili kuongeza mvuto na hadhi ya maeneo ya mijini.

*Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Katika Ngazi ya Jamii*

Mradi huu una lengo la kuimarisha uwezo wa jamii na maeneo mbalimbali katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kujitokeza kwa kasi. Mradi unatambua umuhimu wa ushiriki wa wananchi katika kubuni na kutekeleza mikakati endelevu ya kukabiliana na changamoto hizo, kupitia mbinu shirikishi, elimu ya mazingira pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa. Utekelezaji wa mradi huu unalenga kuimarisha ustahamilivu wa jamii dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi na kuchochea maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2026/2027 umepangiwa jumla ya TZS 5.64 bilioni.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kuanzisha na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji pamoja na kuanzisha jumuiya za watumiaji maji;
ii. Utoaji wa mafunzo kwa wanajamii kuhusu uendeshaji na matengenezo ya mabwawa ya kuvunia maji ya mvua pamoja na usimamizi wa vyanzo vya maji;
iii. Kuwezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa utoaji wa mitaji, vifaranga vya kuku, vifaa vya ufugaji na uanzishwaji wa miradi ya ufugaji; na
iv. Uratibu wa shughuli za mradi.

### *5.3.1 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar*

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ina jukumu la kusajili na kutoa vyeti vya matukio muhimu ya kijamii, ikiwemo vizazi, vifo, ndoa na talaka, pamoja na kusimamia utoaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Kwa mwaka 2026/2027, Wakala umepanga kutekeleza miradi miwili (2) ya maendeleo yenye jumla ya gharama ya TZS 4.26 bilioni, ambapo TZS 4.00 bilioni zitatokana na Serikali na TZS 257.25 milioni zitatokana na Washirika wa Maendeleo.

***Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar***

Mradi una lengo la kuweka miundombinu ili kuimarisha utoaji wa huduma, vituo vya utoaji wa huduma za jamii katika maeneo ya mijini na vijijini kwa kuhakikisha huduma zinapatikana kwa urahisi kwa wananchi wote. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali kwa mwaka 2026/2027,mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.64 bilioni.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kukamilisha ujenzi wa Afisi ya Usajili Wilaya ya Kaskazini 'B' Mahonda Unguja.

***Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii***

Mradi huu una lengo la kuimarisha mifumo ya usajili wa matukio ya kijamii ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma wa usajili wa vizazi, vifo, ndoa na talaka na kupunguza upotevu wa kumbukumbu, kuimarisha usalama wa taarifa za wananchi na kuwapunguzia gharama na muda wa kupata huduma sambamba na kupata takwimu sahihi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya huduma za jamii. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 2.62 bilioni, (TZS 2.36 bilioni kutoka Serikali na TZS 257.25 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali*

i. Kuimarisha na kuboresha mfumo wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi;
ii. Kuimarisha mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii, ikijumuisha uboreshaji wa uwezo wa kuhifadhi na kusimamia kumbukumbu za vifo kwa njia ya kidijitali;
iii. Kuanzisha kituo cha urejeshaji wa huduma baada ya majanga (Disaster Recovery Center) kwa ajili ya kuhakikisha mwendelezo wa mifumo ya usajili; na
iv. Kusajili watoto wenye umri chini ya miaka mitano ili kuongeza wigo wa usajili wa vizazi.

*Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo*

- Kujenga uwelewa, ufuatiliaji na tathmini ya usajili wa vizazi na vifo.

### 5.3.2 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)

Kikosi kina lengo la kuhakikisha usalama wa rasilimali za bahari, kulinda uchumi wa Taifa dhidi ya upotevu unaosababishwa na biashara haramu, na kuimarisha nidhamu na ufanisi wa kijeshi katika kulinda mamlaka ya nchi. Kwa mwaka 2026/2027 Kikosi kimepanga kutekeleza mradi mmoja utakaogharimu jumla ya TZS 12.78 bilioni kutoka Serikalini.

*Mradi wa Kuimarisha Shughuli za Uzamiaji na Uokozi Baharini*

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha uwezo wa kukabiliana na majanga ya baharini katika ukanda wa bahari ya hindi, hususan katika maeneo ya Unguja na Pemba. Mradi unalenga kupunguza athari zitokanazo na ajali za vyombo vya usafiri wa baharini, ikiwemo kuzama kwa meli za abiria na mizigo pamoja na vyombo vingine vya usafiri wa majini. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuongeza ufanisi wa operesheni za uokozi, kuimarisha usalama wa abiria na mali zao, pamoja na kuchangia katika ustawi wa shughuli za kiuchumi zinazotegemea usafiri wa baharini. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2026/2027 umepangiwa jumla ya TZS 12.78 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ununuzi wa meli 'Landcraft';
ii. Kukamilisha ujenzi wa vituo vya uzamiaji na uokozi Ukunjwi - Pemba na Kizimkazi - Unguja; na
iii. Ununuzi wa vipuri.

### *5.3.3 Kikosi cha Valantia*

Kikosi kina jukumu la kudumisha amani, ulinzi na usalama katika Mikoa, Wilaya na Shehia. Kutoa huduma ya ulinzi kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taasisi nyengine za ulinzi na usalama za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mwaka 2026/2027, Kikosi kimepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo utakaogharimu jumla ya TZS 6.40 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Mahanga ya KVZ***

Mradi unatekeleza azma ya Serikali ya kuwa na Idara Maalum za SMZ zenye majengo mazuri yatakayoimarisha utendaji kazi kwa wafanyakazi wake. Kwa mwaka 2026/2027 mradi unalenga kutumia TZS 6.40 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha ujenzi wa hospitali katika kambi ya Mtoni; na
ii. Ununuzi wa samani na vifaa tiba vya hospitali.

### *5.3.4 Chuo Cha Mafunzo*

Chuo kina jukumu la kukuza maadili mema, nidhamu, uwajibikaji, weledi pamoja na kurekebisha tabia za wanafunzi ili kuwaandaa kuwa raia wema, wenye uzalendo na mchango chanya kwa Taifa. Chuo hichi kinatoa elimu ya vitendo na ujuzi wa kitaalamu unaowawezesha wanafunzi kumudu kutekeleza majukumu mbalimbali katika taaluma zao, pamoja na kujiajiri na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Vile vile, Chuo kinaweka mazingira bora na salama ya kufanyia kazi kwa watendaji na askari, ili kuongeza ufanisi, nidhamu na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa mwaka 2026/2027, Chuo kimepanga

kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo wenye jumla ya gharama ya TZS 3.40 bilioni, kutoka Serikalini.

***Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga***

Mradi huu unatekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha watendaji wa Chuo cha Mafunzo wanapata makaazi bora na salama, pamoja na kuwepo kwa mazingira mazuri na wezeshi ya kufanyia kazi, ili kuongeza ufanisi, uwajibikaji na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.40 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya Ubago na Tungamaa;
ii. Kukamilisha ujenzi wa nyumba nne (mbili Ubago na mbili Kinumoshi) pamoja na ukarabati wa nyumba mbili Kengeja;
iii. Kufanya ukarabati wa vyuo vya urekebishaji tabia katika kambi ya Tungamaa, Kengeja, Kinumoshi na Ubago; na
iv. Kukamilisha uzio katika kambi ya Bumbwini.

### *5.3.5 Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)*

Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) lina majukumu ya msingi ya kutoa mafunzo ya uzalendo, nidhamu na maadili mema kwa vijana; kuendeleza ujuzi wa kiufundi na ujasiriamali; kuongeza uzalishaji kupitia miradi ya kilimo na mifugo; kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo; pamoja na kuchangia juhudi za Serikali za kupunguza ukosefu wa ajira kupitia mafunzo ya stadi za kazi. Kwa mwaka 2026/2027, Kikosi kimepangiwa jumla ya TZS 12.76 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza miradi miwili (2) ya maendeleo.

***Mradi wa Ujenzi wa Dakhalia***

Mradi una lengo la kutoa huduma ya malazi kwa wanafunzi wanaoishi mbali na maeneo yao ya makaazi. Dakhalia itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu na

kulinda usalama wa wanafunzi dhidi ya unyanyasaji. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 8.52 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuendelea na ujenzi wa dakhalia ya skuli ya sekondari JKU - Mtoni.

***Mradi wa Uimarishaji wa Utoaji wa Huduma za Wakala wa Ulinzi JKU***

Mradi una lengo la kuimarisha uwezo wa kulinda raia na mali zao katika maeneo tofauti ikiwemo Taasisi za Serikali, biashara na makaazi binafsi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 4.24 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuendelea na ujenzi wa Afisi za Wakala wa Ulinzi wa JKU - Mtoni.

### *5.3.6 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi*

Kikosi kina jukumu la kulinda maisha ya wananchi, mali zao na mazingira kwa kutoa huduma za haraka na za kitaalamu za kuzima moto na uokozi katika matukio ya dharura na majanga mbalimbali. Aidha, Kikosi kinahusika na kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu kinga na udhibiti wa ajali za moto, kufanya ukaguzi wa usalama wa majengo na maeneo ya umma, pamoja na kuandaa na kuratibu mipango ya maandalizi na mwitikio wa dharura kwa kushirikiana na Taasisi husika, ili kuimarisha usalama na ustahamilivu wa jamii dhidi ya majanga.

Kwa mwaka 2026/2027, Kikosi kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 7.56 bilioni (TZS 4.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 3.56 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari***

Mradi huu unatekeleza malengo ya Serikali ya kuhakikisha Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kinapata Afisi bora, za kisasa, salama na zenye mazingira wezeshi ya kufanyia kazi. Aidha, mradi huu unalenga kuimarisha mazingira ya kazi ili kuwawezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 4.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na ujenzi wa Afisi Kuu Chanjani - Pemba;
ii. Ununuzi na ufungaji wa mifumo ya mawasiliano; na
iii. Kuendelea na ujenzi wa kituo cha zimamoto eneo la Mji wa Michezo - Fumba.

***Mradi wa Ununuzi wa Magari na Vifaa vya Kuzimia Moto***

Mradi huu una lengo la kuimarisha uwezo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa na vya kutosha kwa ajili ya kutoa huduma za uokozi kwa ufanisi. Mradi huu inalenga kuwezesha uokoaji wa haraka wa maisha ya wananchi na kulinda mali zao pindi zinapotokea ajali za moto na majanga mengine. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.56 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Ununuzi wa vifaa vya kisasa na magari maalum kwa ajili ya utoaji wa huduma za uokozi na uzimaji moto.

## 5.4 Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais

Afisi ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa maeneo mtambuka yakiwemo mazingira, masuala ya watu wenye ulemavu, UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya. Aidha, Afisi imepewa dhamana ya kuhakikisha mshikamano wa kitaifa, uratibu wa kisera na ushirikiano na taasisi mbalimbali za Serikali katika utekelezaji wa ajenda za maendeleo endelevu.

Kwa mwaka 2026/2027, Afisi imepanga kutekeleza miradi minne (4) ya maendeleo yenye jumla ya gharama ya TZS 7.11 bilioni, (TZS 5.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 2.11 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kutathmini na kupunguza athari za maeneo yaliyo hatarini kutokana na mabadiliko ya tabianchi, pamoja na kuchukua hatua mahsusi za kuhimili na kudhibiti athari za mabadiliko hayo hususan katika ukanda wa pwani. Utekelezaji wa mradi unatarajiwa kuimarisha uhimilivu wa jamii dhidi ya athari za tabianchi na kuchangia katika uhifadhi endelevu wa mazingira. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 5.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Urejeshaji wa uoto wa asili kupitia upandaji wa miti na uhifadhi wa maeneo yaliyoharibiwa; na
ii. Ujenzi wa urejeshaji wa maeneo ya fukwe yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi.

***Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za Pwani ya Zanzibar***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha uwezo wa jamii za pwani ya Zanzibar kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa njia endelevu na shirikishi. Utekelezaji wa mradi unalenga kuongeza ustahamilivu wa jamii, kulinda mazingira ya pwani na kuimarisha usalama wa rasilimali za asili. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 1.41 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shuguli Zilizopangwa kutekelezwa***

i. Ujenzi wa miundombinu ya udhibiti wa mmong'onyoko wa udongo, katika maeneo ya Bumbwini Mafufuni na Kiongwe Kidogo;
ii. Urejeshaji wa uoto wa asili na uhifadhi wa mazingira kupitia upandaji wa miti pamoja na uanzishaji na uimarishaji wa vitalu vya mikoko na miti mingine;

iii. Ujenzi wa visima na makinga maji katika eneo la Tovuni – Pemba, pamoja na kuimarisha uelewa wa jamii kuhusu usimamizi wa pamoja wa vyanzo vya maji; na
iv. Kusaidia wakulima kuanzisha mashamba darasa na kufanya kilimo cha majaribio katika maeneo yenye changamoto ya udongo wa chumvi.

***Mradi wa Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Tanzania (Scale)***

Mradi huu una lengo la kuimarisha uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa katika kupanga, kuratibu na kutekeleza hatua madhubuti za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kuongeza ustahamilivu wa jamii, kulinda mazingira na kuhakikisha maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 551.78 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kukuza mfumo wa Kitaifa na Serikali za Mitaa katika kusimamia hatari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi na hatua za kukabiliana nayo.

***Mradi Shirikishi wa Kuhimili Mifumo ya Ikolojia ya Bahari na Ukanda wa Pwani na Shughuli za Kujipatia Kipato***

Mradi huu una lengo la kuimarisha ustahimilivu wa mifumo ya ikolojia ya bahari na ukanda wa pwani pamoja na kuboresha uwezo wa jamii za eneo la Kusini Mashariki Pemba, kujipatia kipato kwa njia endelevu ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na pwani. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 153.79 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuimarisha mifumo ya ikolojia ya bahari na ukanda wa pwani ili kuboresha maisha ya jamii na mazingira.

### *5.4.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA)*

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar ni Taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria na kupewa jukumu la kuhakikisha kuwa mazingira ya Zanzibar yanatunzwa, yanahifadhiwa na yanaendelezwa kwa njia endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo. Mamlaka hii inahusika na kuratibu, kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na mikakati ya usimamizi wa mazingira pamoja na kuhakikisha uzingatiaji wa viwango vya ulinzi wa mazingira katika shughuli zote za maendeleo. Kwa mwaka 2026/2027, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira imepanga kutekeleza miradi mitatu (3) itakayogharimu jumla ya TZS 2.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani***

Lengo la mradi huu ni kuchochea na kuimarisha jitihada za kujenga Zanzibar ya kijani kupitia uhifadhi endelevu wa mazingira, ongezeko la uoto wa asili na ule uliopandwa, pamoja na kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za asili ili kuboresha ustawi wa jamii na kulinda mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Uhamasishaji wa jamii kuhusu Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani;
ii. Ununuzi na usambazaji wa mbegu na miche kwa ajili ya vitalu vya miti; na
iii. Uandaaji wa Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani na Mkakati wa Mawasiliano.

***Mradi wa Mfumo wa Kitaifa wa Taarifa za Usimamizi wa Mazingira***

Mradi una lengo la kuandaa mfumo utakaokusanya, kuhifadhi, kuchambua na kusambaza taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu hali ya mazingira nchini. Mfumo huu utasaidia kuimarisha uratibu wa Taasisi mbalimbali zinazohusika na masuala ya mazingira kwa kuwezesha upatikanaji wa takwimu na taarifa zinazohitajika katika kufanya maamuzi, upangaji wa sera na ufuatiliaji wa utekelezaji wa

miradi ya mazingira. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendeleza mfumo wa kidigitali wa tathmini ya mazingira na utoaji wa vibali pamoja na moduli za mfumo wa ufuatiliaji wa mazingira; na
ii. Ununuzi wa miundombinu ya TEHAMA na usimamizi wa taarifa za mazingira.

***Mradi wa Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Tanzania (Scale)***

Mradi huu una lengo la kuimarisha uwezo wa mamlaka za Serikali za mitaa katika kupanga, kuratibu na kutekeleza hatua madhubuti za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kuongeza ustahimilivu wa jamii, kulinda mazingira na kuhakikisha maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 111.98 Milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandaa na kutekeleza orodha ya ukaguzi kwa ajili ya miradi midogo ya 'Scale';
ii. Kuandaa na kutekeleza muongozo wa ufuatiliaji wa mazingira kwa ajili ya mradi wa 'Scale'; na
iii. Kusaidia uratibu wa mradi.

### *5.4.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya*

Mamlaka inajukumu la kuratibu, kusimamia na kutekeleza sera, mipango na mikakati ya kudhibiti matumizi na usambazaji wa madawa ya kulevya Zanzibar. Utekelezaji wa majukumu haya unachangia moja kwa moja katika kulinda afya ya jamii, kuimarisha usalama wa raia pamoja na kupunguza athari hasi za kijamii na kiuchumi hususan kwa vijana ambao ni rasilimali muhimu katika

maendeleo ya Taifa. Katika mwaka 2026/2027, Mamlaka imepanga kutekeleza mradi mmoja (1) wa maendeleo wenye thamani ya TZS 8.25 bilioni, kutoka Serikalini.

***Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya***

Mradi huu unalengo la kutoa tiba na marekebisho ya tabia kwa wanaotaka kuachana na matumizi ya dawa za kulevya. Kwa mwaka 2026/2027 mradi umepangiwa kutumia TZS 8.25 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia, Kangagani-Pemba.

### 5.5 Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi

Afisi ina dhamana ya kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na kuratibu masuala ya Muungano kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kuzingatia misingi ya Katiba, sheria na kanuni husika. Aidha, Afisi ina jukumu la kuimarisha utawala bora, kulinda na kuendeleza haki za binadamu pamoja na kuhakikisha ushirikishwaji mpana wa wadau katika mchakato wa maendeleo. Majukumu haya yanatekelezwa kwa kuzingatia nguzo ya utawala bora na Taasisi imara ambayo inalenga kujenga Serikali yenye ufanisi, uwajibikaji, uwazi na inayotoa huduma bora kwa wananchi. Kupitia uratibu madhubuti wa shughuli za Serikali na masuala ya Muungano, Afisi inachangia moja kwa moja katika kuimarisha mshikamano wa Kitaifa, utulivu wa kisiasa na mazingira wezeshi ya ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu.

Kwa mwaka 2026/2027, Afisi imepanga kutekeleza programu moja (1) ya kimkakati itakayogharimu jumla ya TZS bilioni 40.00, kutoka kwa kwa Washirika wa Maendeleo.

**Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Nne (TASAF IV)**

Mpango huu unatekelezwa kwa lengo la kuziwezesha kaya zenye kipato cha chini sana kuongeza kipato, kupanua fursa za kiuchumi na kuimarisha uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu ya kibinadamu, hususan chakula, afya na elimu. Aidha, mpango unalenga kuchochea uwezeshaji wa jamii kupitia utekelezaji wa miradi inayoibuliwa na wananchi katika sekta za elimu, afya pamoja na utoaji wa ajira za muda mfupi. Utekelezaji wa programu hii ni nguzo muhimu ya maendeleo jumuishi ya kijamii na kupunguza umasikini, inayolenga kuinua hali ya maisha ya wananchi, kupunguza pengo la kipato na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za msingi kwa wote. Kupitia TASAF IV, Serikali inaimarisha mtaji wa watu, kuongeza uhimilivu wa kaya maskini dhidi ya mishtuko ya kiuchumi na kuweka msingi wa ushiriki wao katika uchumi wa kisasa na endelevu. Kwa mwaka 2026/2027, Mpango huu umepangiwa jumla ya TZS bilioni 40.00, kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na uhaulishaji wa fedha kwa kaya za walengwa wa TASAF; na
ii. Kuanza utekelezaji wa ujenzi wa miradi midogo ya kijamii itakayoibuliwa na wananchi, hususan katika sekta za elimu, maji na afya.

### *5.6 Wizara ya Afya*

Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu sekta ya afya kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kinga, tiba na uimarishaji wa afya ya jamii, sambamba na kutoa miongozo na maelekezo ya kitaalamu ili kujenga jamii yenye afya bora na yenye tija ili kuweza kuimarisha uwezo katika utoaji wa huduma bora, salama na zenye usawa kwa wananchi wote. Majukumu haya yanatekelezwa kwa kuzingatia maendeleo ya rasilimali watu na ustawi wa jamii, inayolenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya, kuongeza matarajio ya maisha na kuimarisha ustahaimilivu wa jamii dhidi ya magonjwa na changamoto za kiafya.

Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu nane (8) na miradi mitatu (3) ya maendeleo yenye jumla ya gharama ya TZS 203.76 bilioni. (TZS 100.52 bilioni kutoka Serikalini na TZS 103.24 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar**

Programu ina lengo la kutokomeza maradhi ya malaria kwa kuhakikisha kwamba maradhi haya yanamalizika hapa Zanzibar. Aidha, programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2026/2027 programu imepangiwa jumla ya TZS 8.69 bilioni (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 7.69 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Uratibu na usimazi wa uendeshaji wa shughuli za malaria;
ii. Utumiaji wa taarifa na ufuatiliaji wa wagonjwa katika hospitali, vituo na majumbani; na
iii. Ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa wa malaria;

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Uratibu na usimazi wa uendeshaji wa shughuli za malaria;
ii. Utumiaji wa taarifa na ufuatiliaji wa wagonjwa katika hospitali, vituo na majumbani;
iii. Kuimarisha uchunguzi na matibabu ya ugonjwa wa malaria katika hospitali na vituo vya afya;
iv. Ufuatiliaji wa mwenedo wa ugonjwa wa malaria; na
v. Uthibiti wa mbu waenezao ugonjwa wa malaria.

**Programu ya Shirikishi ya UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma**

Programu ina lengo la kupambana na maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma. Lengo kuu ni kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya

Ukimwi, vifo vitokanavyo na maradhi ya kifua Kikuu, homa ya Ini na kupunguza maambukizi ya Ukoma. Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 5.63 bilioni (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.63 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kuimarisha huduma za matibabu kwa watu na makundi maalum wanaoishi na VVU;
ii. Kuimarisha utoaji wa huduma za kinga na tiba ya homa ya Ini katika jamii;
iii. Uhamasishaji na kuongeza uelewa katika jamii, juu ya kinga dhidi ya maambukizi ya Ukimwi, magonjwa ya kujamiana, homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma;
iv. Kufanya uhamasishaji kwa wanaume juu ya upimaji wa virusi vya ukimwi wakati wa mahudhurio ya kliniki;
v. Kuimarisha huduma za kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto; na
vi. Uratibu na usimamizi wa kazi za programu.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kuimarisha huduma za matibabu kwa watu na makundi maalum wanaoishi na VVU;
ii. Uhamasishaji na kuongeza uelewa katika jamii, juu ya kinga dhidi ya maambukizi ya Ukimwi, magonjwa ya kujamiana, homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma;
iii. Uratibu na usimamizi wa kazi za programu; na
iv. Kuimarisha huduma za kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

**Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto**

Programu ina lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2026/2027, TZS 5.32 bilioni zimetengwa (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.32 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Uratibu na usimamizi wa huduma za afya ya mama na mtoto;
ii. Kuimarisha matibabu mjumuisho ya watoto chini ya miaka mitano pamoja na kuboresha matumizi ya muongozo wa matibabu ya watoto;
iii. Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza matatizo yatokanayo na vifo vya mama na mtoto pamoja na kutoa elimu juu ya athari za mimba za utotoni; na
iv. Kuimarisha huduma za damu salama kwa mama wajawazito na watoto.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Ukarabati wa kona rafiki za afya kwa vijana, ununuzi wa chanjo, dawa na vifaa tiba;
ii. Kutoa taaluma juu ya wajibu wa wanaume katika huduma za uzazi wa mpango;
iii. Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza matatizo yatokanayo na vifo vya mama na mtoto;
iv. Kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo ya mama na mtoto;
v. Uratibu na usimamizi wa huduma za afya ya mama na mtoto;
vi. Kuimarisha huduma za mama na watoto chini ya umri wa miaka mitano;
vii. Ukarabati na uwekaji wa vifaa katika vituo vya mkono kwa mkono kutokana na kujikinga na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto katika Mikoa mitatu;

viii. Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza matatizo yatokanayo na vifo vya mama na mtoto; na
ix. Kuimarisha huduma za damu salama kwa mama wajawazito na watoto.

**Programu ya Kuimarisha Huduma za Mama na Mtoto**

Programu hii inalenga kuboresha afya na ustawi wa mama na mtoto kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya. Programu inajikita katika kuimarisha miundombinu ya afya, upatikanaji wa vifaa na dawa muhimu, pamoja na kuongeza uwezo wa watumishi wa afya ili kupunguza vifo vya mama na mtoto na kuongeza matumizi ya huduma za afya, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa. Kwa mwaka 2026/2027, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 23.40 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa mradi;
ii. Ujenzi wa vituo vya afya – Fuoni na Jang'ombe - Unguja
iii. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi hospitali ya Wilaya ya Micheweni - Pemba na Kivunge - Unguja; na
iv. Kusomesha madaktari wa fani maalum.

**Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya**

Programu inalenga kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa kukarabati vituo vya kutolea huduma ili kukidhi viwango vya Kitaifa. Utekelezaji wake unatarajiwa kuongeza ufanisi wa utoaji huduma, kupunguza msongamano kwa wagonjwa, na kuboresha hali ya afya ya jamii. Kwa mwaka 2026/2027 programu inatarajia kugharimu jumla ya TZS 47.67 bilioni (TZS 34.81 bilioni kutoka Serikalini TZS 12.86 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa fedha za Serikali***

i. Kuendelea na ujenzi wa hospitali ya Mkoa wa Kaskazini – Unguja;
ii. Kuanza ujenzi wa hospitali ya Mkoa wa Kusini - Unguja, Kaskazini na Kusini – Pemba;

iii. Ujenzi wa Maabara ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi, Chamanangwe – Pemba; na
iv. Ujenzi wa Kituo cha Usimamizi na Udhibiti wa Maradhi ya Mripuko.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo

i. Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Kusini Unguja;
ii. Ujenzi wa hospitali ya Mkoa wa Kaskazini na Kusini – Pemba.

**Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi**

Programu ina lengo la kuimarisha afya ya msingi kwa kuimarisha miundombinu ya vituo vya afya ya msingi ili viweze kutoa huduma za afya ya msingi zenye kiwango na kuimarisha afya ya jamii. Programu hii inatekelezwa na Serikali ambapo kwa mwaka 2026/2027 imepangiwa jumla ya TZS 40.05 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na ujenzi wa zahanati 10; na
ii. Kuendeleza ujenzi wa vituo vya afya ya msingi 50 Unguja na Pemba.

**Programu ya Jamii ni Afya**

Program hii ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya karibu na wananchi kwa kuwapelekea wahudumu za afya katika ngazi ya shehia ili waweze kusaidia wananchi huduma za awali. Kwa mwaka 2026/2027 jumla ya TZS 3.00 bilioni zimetengwa (TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kutoka Serikalini***

i. Kuongeza idadi na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ngazi ya jamii;
ii. Uratibu wa shughuli za wahudumu wa afya wa jamii; na
iii. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini wa kazi za wahudumu wa afya ngazi ya jamii;

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kutoka Washirika wa Maendeleo***

- Uratibu wa shughuli za wahudumu wa afya ya jamii.

**Programu ya Kuimarisha Nguvu Kazi Katika Sekta ya Afya**

Program ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa madaktari bingwa na bobezi ili kuimarisha huduma za matibabu katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Rufaa. Kwa mwaka 2026/2027, Programu hii imepangiwa jumla ya TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kusomesha madaktari bingwa na wabobezi katika fani za afya;

***Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.***

Mradi una lengo la kuimarisha huduma katika hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa. Kupitia mradi huu Serikali imepanga kufanya ukarabati katika hospitali ya Mnazi mmoja ili kuiwezesha kutoa huduma nzuri na zenye kukidhi mahitaji. Kwa mwaka 2026/2027, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 60.89 bilioni (TZS 15.70 bilioni kutoka Serikalini na TZS 45.19 kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli ilizopangwa Kutekelezwa kwa fedha za Serikali***

- Ukarabati wa hospitali ya Mnazi Mmoja.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa fedha za Washirikaw a Maendeleo***

i. Ukarabati na utanuzi wa hospitali ya Mnazi Mmoja; na
ii. Usimamizi wa mradi.

***Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia Binguni***

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya Rufaa kwa kiwango cha kibingwa na bobezi sambamba na kuimarisha huduma za kufundishia taaluma za afya. Kwa mwaka 2026/2027 mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 6.11 bilioni (TZS 1.97 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.14 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

- Usimamizi wa ujenzi katika hospitali ya Binguni.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

- Ujenzi wa majengo ya hospitali ya Binguni.

***Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Kidigitali***

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa taarifa za afya na kuhakikisha taarifa zote za afya zinapatikana kwenye mfumo mama wa taarifa ili ziweze kutumika katika utungaji wa sera, uandaaji wa miongozo na utoaji wa maamuzi katika ufuatiliaji wa mienendo ya maradhi kwa lengo la kupunguza vifo na kukabiliana na maradhi ya miripuko. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuendelea na uimarishaji wa mifumo ya kidigitali kwa afya katika ngazi zote.

### 5.6.1 Hospitali ya Mnazi Mmoja

Hospitali hii imeanzishwa kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, kutoa huduma za rufaa pamoja na kuimarisha matibabu ya kibingwa katika sekta ya afya. Kupitia uwepo wa madaktari bingwa, vifaa tiba vya kisasa na miundombinu ya hospitali, Mnazi Mmoja imeendelea kuwa nguzo muhimu katika utoaji wa huduma za afya zenye ubora, usalama na ufanisi kwa wananchi wote. Aidha, hospitali hutoa huduma za dharura, upasuaji, mama na mtoto, maabara pamoja na mafunzo kwa wataalamu wa afya ili kuimarisha maendeleo ya sekta ya afya nchini. Kwa mwaka 2026/2027, Taasisi imepanga kutumia jumla ya TZS 3.00 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mmoja wa maendeleo.

***Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Macho***

Mradi unalenga kuboresha miundombinu, vifaa tiba na huduma za kibingwa ili kuongeza ubora wa huduma za afya, kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya

Zanzibar na kuboresha ustawi wa wananchi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 3.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Ujenzi wa hospitali ya macho – Mazizini.

## 5.7 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu matumizi bora, yenye tija na endelevu ya ardhi kwa lengo la kuzuia migogoro, kudhibiti matumizi holela, na kulinda mazingira sambamba na kuendeleza ustawi wa kijamii na kiuchumi. Aidha, Wizara inasimamia maendeleo ya miji na makaazi kwa kuzingatia viwango vya kisasa vya upangaji miji na ujenzi wa miundombinu, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii, usalama na mazingira rafiki ya afya. Majukumu haya yanatekelezwa kwa kuzingatia maendeleo ya miji na makaazi endelevu, inayolenga kujenga miji jumuishi, salama, himilivu na yenye ushindani wa kiuchumi.

Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutumia jumla ya TZS bilioni 300.92 kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa programu moja ya maendeleo.

**Programu ya Ujenzi wa Nyumba na Uimarishaji wa Miji**

Programu inalenga kuboresha miundombinu na huduma za mijini ili kuimarisha ustawi wa wakaazi na kukuza maendeleo endelevu ya miji. Kupitia utekelezaji wake, inatarajiwa kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi, kupunguza msongamano wa watu mijini, kudhibiti uchafuzi wa mazingira, na kuifanya miji kuwa salama, nadhifu na yenye kuvutia kwa uwekezaji. Programu hii pia ina mchango mkubwa katika kujenga miji jumuishi na himilivu, inayoweza kukabiliana na changamoto za ukuaji wa kasi wa miji. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa kiasi cha TZS 300.92 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

- i Kuendelea na ujenzi wa nyumba za makaazi katika eneo la Chumbuni, Saateni, Kikwajuni, Kisakasaka na Mabaoni;
- ii Kuendeleza Miji ya Kale na maeneo ya ng'ambo (Kwahani, Shaurimoyo na Mwembeshauri); na
- iii Kuimarisha maeneo ya pembezoni mwa barabara kuu (Uwanja wa Ndege-Amani, Kiembesamaki- Mnazi Mmoja, Chukwani - Mazizini, Amani - Kwabiziredi na Fumba - Kiembesamaki).

## 5.8 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Wizara ina lengo la kukuza viwanda vidogo vidogo na vya kati sambamba na kuimarisha mazingira ya kufanya biashara, ili kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu mbili kwa gharama ya TZS 34.26 bilioni kutoka Serikalini.

### Programu ya Kuendeleza Viwanda

Programu hii ina lengo la kukuza uchumi kupitia uimarishaji wa sekta ya viwanda na mazingira mazuri ya biashara ili kuongeza uzalishaji wa ndani, kuimarisha thamani ya mazao, na kuongeza ajira. Pia inalenga kuboresha miundombinu, kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kukuza matumizi ya teknolojia za kisasa ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 25.74 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

- i. Ujenzi wa majengo sita (6) (Dunga 4 na Chamanangwe 2) ya viwanda vidogo na vya kati;
- ii. Ujenzi wa uzio maeneo ya viwanda Dunga - Unguja na Chamanangwe – Pemba;
- iii. Ujenzi wa barabara na miundombinu ya maji katika maeneo ya viwanda Chamanangwe - Pemba; na
- iv. Uendeshaji na usimamizi wa miradi ya Dunga na Chamanangwe.

**Programu ya Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Dimani - Zanzibar**

Mradi huu una lengo la kutoa huduma za kuimarisha sekta ya biashara na viwanda kwa kutoa msaada kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 8.52 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa kumbi mbili (2) za maonesho; na
ii. Ujenzi wa mikahawa ya kisasa katika eneo la maonesho.

## 5.9 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Wizara ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa elimu jumuishi, bora na yenye usawa kwa wananchi wote, kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya juu pamoja na mafunzo ya amali yanayolenga kukuza ujuzi wa vitendo na ajira kwa jamii. Kwa kutambua umuhimu wa elimu katika maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia, Wizara imeweka mikakati na sera madhubuti zinazolenga kuboresha ubora wa elimu kwa kuimarisha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia pamoja na kuongeza uwezo wa walimu na wakufunzi. Aidha, Wizara inaendeleza mafunzo ya amali ili kuwajengea vijana stadi zinazokidhi mahitaji ya soko la ajira na kuchochea ubunifu na ujasiriamali.

Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu moja (1) na miradi miwili (2) ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 711.07 bilioni (TZS 466.08 bilioni kutoka Serikalini na TZS 244.99 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu**

Programu ina lengo la kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu. Hivyo, inajikita katika ujenzi, ukarabati na upanuzi wa majengo ya skuli ili kuweka mazingira bora ya kujifunzia. Aidha, Programu imeanzishwa ili kuondoa utaratibu wa wanafunzi kuingia skuli kwa zamu na kuwa

na mkondo mmoja, uwepo wa maabara za kutosha, maktaba na miundombinu ya TEHAMA. Programu inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 598.41 bilioni (TZS 355.18 bilioni kutoka Serikalini na TZS 243.23 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kujenga madarasa 1,600 kupitia skuli 20 za kisasa za maandalizi, tano (5) za ghorofa za msingi, 10 za ghorofa za sekondari, mbili (2) za sekondari za wanawake na tano (5) za sekondari za amali;
ii. Kuendelea na ujenzi wa skuli tatu (3) zenye dakhalia kwa Mashirikiano na BADEA;
iii. Kufanya ukarabati wa madarasa chakavu na ukamilishaji wa madarasa yaliyoanzishwa na wananchi.
iv. Kujenga vyoo 800 na sehemu za kunawia mikono kwa skuli za maandalizi, msingi na sekondari;
v. Kujenga karakana moja (1) kila Wilaya ili kuwezesha utoaji wa mafunzo ya amali na ufundi kwa wanafunzi wa sekondari;
vi. Kujenga viwanja vya michezo katika skuli za michepuo ya michezo Unguja na Pemba na kuzipatia vifaa;
vii. Kufanya ukarabati wa vituo vya elimu mbadala na watu wazima Rahaleo, Forodhani na jengo la Afisi Pemba;
viii. Ujenzi wa jengo la Afisi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali;
ix. Kuanza ujenzi wa vyuo vya Mafunzo ya Amali pamoja na kuvipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia;
x. Ujenzi wa majengo ya utawala na taaluma ikiwemo Chuo cha ubaharia, skuli ya elimu na lugha, skuli ya afya na kliniki ya meno, skuli ya biashara, Taasisi ya utalii, dakhalia, kituo cha huduma kwa wanafunzi, nyumba za wafanyakazi na viwanja vya michezo katika Chuo cha Taifa cha Zanzibar;

xi. Kujenga ukumbi, dakhalia ya wanawake na karakana katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume - Unguja; pamoja na Jengo la utawala, Afisi za walimu, madarasa, maabara na karakana kwa Pemba;

xii. Ujenzi wa majengo ya utawala, madarasa, maabara, nyumba za walimu na migahawa katika Chuo cha Teknolojia cha India (IIT Madras);

xiii. Ujenzi wa Afisi ya Baraza la Mitihani na Kituo cha kuchapisha mitihani Kisakasaka, Afisi mbili (2) za Elimu na Ukaguzi za Mikoa;

xiv. Ujenzi wa nyumba za walimu; na

xv. Ukarabati wa jengo la Afisi na ujenzi wa ghala Mazizini-Unguja.

***Shuguli zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kujenga madarasa 1,600 kupitia skuli maandalizi, msingi na sekondari,

ii. Kujenga vyoo 800 na sehemu za kunawia mikono kwa skuli za maandalizi, msingi na sekondari;

iii. Kujenga skuli mbili (2) za ufundi ili kuwajengea vijana ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko la ajira;

iv. Kuanza ujenzi wa vyuo vya Mafunzo ya Amali pamoja na kuvipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

v. Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ubaharia;

vi. Ujenzi jengo jipya la utawala, skuli ya elimu na lugha, Kituo cha huduma kwa wanafunzi, nyumba za wafanyakazi na viwanja vya michezo katika Kampasi ya Tunguu;

vii. Kujenga dakhalia ya wanawake na karakana katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume - Unguja; pamoja na jengo la utawala, afisi za walimu, madarasa, maabara na karakana kwa Pemba; na

viii. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Afisi Mazizini – Unguja na Chake Chake Pemba na ununuzi wa samani za Afisi.

***Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia***

Mradi una lengo la kuhakikisha upatikanaji wa vifaa bora, vya kutosha na kisasa vya kujifunzia na kufundishia ili kuboresha ubora wa elimu katika

ngazi zote. Aidha, mradi unazingatia umuhimu wa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha ufundishaji na ufunzaji, ikiwa ni pamoja na matumizi ya vifaa vya kidijitali. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 67.66 bilioni (TZS 65.90 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.76 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo)

***Shuguli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Ununuzi wa samani za skuli (viti na meza), vifaa vya maabara, maktaba na vifaa vya usafi kwa ajili ya skuli mpya;
ii. Ununuzi wa gari maalum kwa ajili ya Maktaba Tembezi (Mobile Library);
iii. Ununuzi wa samani na vifaa kwa skuli za mafunzo ya amali;
iv. Kuimarisha karakana za kufundishia na kujifunzia kwa kuzipatia vifaa na mashine za kisasa;
v. Kutayarisha na kuchapisha vitabu vya mtaala mpya kwa madarasa ya kidato cha tatu, nne na sita na ununuzi wa vitabu vya maktaba;
vi. Kutoa mafunzo ya matumizi ya mtaala mpya kwa walimu wa kidato cha tatu, nne na sita;
vii. Kutayarisha vifaa vya utekelezaji wa mtaala rekebifu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum;
viii. Uanzishaji wa huduma za maktaba mtandao pamoja na Hifadhi ya Taifa ya Taarifa; na
ix. Kusambaza vifaa ikiwemo vya TEHAMA kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia kwa skuli zote.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Ununuzi wa samani, vifaa vya mafunzo ya amali, utaoji wa mafunzo;
ii. Kutayarisha na kuchapisha vitabu vya mtaala mpya kwa madarasa ya kidato cha tatu, nne na kidato cha sita na ununuzi wa vitabu vya maktaba;
iii. Kutoa mafunzo ya matumizi ya mtaala mpya kwa walimu wa kidato cha tatu, nne na sita;

iv. Kutayarisha vifaa vya utekelezaji wa mtaala rekebifu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
v. Kusambaza vifaa ikiwemo vya TEHAMA kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia kwa skuli zote;
vi. Kuanzisha mfumo wa tathmini ya kitaifa na kufanya tathmini hizo kwa darasa la pili, tatu na kidato cha pili; na
vii. Kuunganisha skuli za msingi na sekondari katika mkonga wa Taifa.

***Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo kuwapatia mikopo itakayowawezesha wanafunzi kuendelea na masomo ya elimu ya juu ili kuongeza idadi ya wataalam, watafiti na wabunifu wazalendo katika kukuza maendeleo ya Taifa. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 45.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shuguli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuwapatia mikopo wanafunzi wa elimu ya juu Zanzibar.

**5.10 Wizara ya Fedha na Mipango**

Wizara ina jukumu la kusimamia fedha za umma, kupanga bajeti, na kuandaa pamoja na kutekeleza mikakati ya maendeleo ya taifa kwa kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa miradi ya maendeleo, usimamizi bora wa rasilimali, na uimarishaji wa ukusanyaji wa mapato na utafutaji fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, Wizara ina wajibu wa kuandaa na kutekeleza sera za kifedha zinazolenga kuchochea ukuaji wa uchumi. Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu nne (4) zitakazogharimu TZS 977.73 bilioni, (TZS 938.06 bilioni zitatokana na Serikali na TZS 39.66 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Ujenzi wa Afisi za Serikali Zanzibar**

Programu hii inalenga kujenga na kukarabati majengo ya Afisi za Serikali ili kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi wa taasisi na idara za umma, pamoja na

kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Serikali kwa lengo la kuongeza ubora wa utoaji huduma kwa wananchi. Aidha, programu hii inahusisha ujenzi wa Afisi mpya za Serikali katika maeneo yaliyopangwa ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za Serikali unakuwa karibu na wananchi, sambamba na uimarishaji wa majengo ya zamani ili kuhakikisha usalama, uimara na uendelevu wa huduma. Kwa mwaka 2026/2027, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 166.96 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha ujenzi wa Afisi za Serikali ikiwemo Mamalaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Shirika la Magazeti, Afisi ya Nyaraka na Chuo cha Utawala wa Umma;
ii. Kuanza ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kiislam-Mazizini, Wakala wa Uchapaji wa Serekali, Tume ya Utangazaji, Afisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na Afisi ya Tume ya Uchaguzi-Pemba; na
iii. Kuendelea na ujenzi wa Mji wa Serikali na Baraza la Wawakilishi katika eneo la Kisakasaka.

**Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)**

Programu hii inalenga kuimarisha miundombinu, huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya Zanzibar. Kwa mwaka 2026/2027, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 32.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.
Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa kituo cha kukusanyia taka Fuoni – Chunga zinazotoka katika vizimba;
ii. Kuendelea na ujenzi wa vizimba vya kukusanyia taka Unguja 61 na Pemba 28;
iii. Ununuzi wa magari 26 ya kubebea taka kwa ajili ya Manispaa za Unguja na Pemba;
iv. Kuendelea na ujenzi wa mradi salama wa watembea kwa miguu katika Mji Mkongwe;

v. Kuendeleza maeneo ya utalii katika vijiji vya Nungwi, Chwaka na Makunduchi – Unguja;
vi. Kuendelea na uandaaji wa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi kwa Kisiwa cha Pemba; na
vii. Kuendelea na uandaaji wa Mfumo wa Utambuzi wa Taarifa za Kijiografia na Maeneo.

**Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)**

Programu hii ina lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma katika utoaji wa huduma ya ukaguzi wa fedha za umma, usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 3.24 bilioni (TZS 700 milioni kutoka Serikalini na TZS 2.54 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Kuwajengea uwezo Maafisa wa Uchumi 12 kuhusu ushirikiano wa Kiuchumi wa Kikanda;
ii. Kuandaa toleo la pili la tovuti ya takwimu za uchumi Zanzibar;
iii. Kuwajengea uwezo Maafisa Mipango ishirini 20 kuhusu uchambuzi wa upembuzi yakinifu kwa programu na miradi ya maendeleo;
iv. Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Programu ya mageuzi katika usimamizi wa fedha za umma;
v. Kukamilisha Tathmini ya uwajibikaji na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma;
vi. Kuandaa mafunzo kwa wafanyakazi 80 kuhusu masuala ya ununuzi wa kijani.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kuandaa, kuboresha na kuunganisha mifumo sita (6) ya usimamizi wa fedha;

ii. Kuandaa na kufanya mapitio ya sheria, sera, kanuni na miongozo inayohusiana masuala mbali mbali ya mapato, matumizi, udhibiti na ukaguzi;
iii. Kuandaa tafiti za masuala ya usimamizi wa mageuzi ya fedha za umma;
iv. Usimamizi na uendeshaji wa mradi; na
v. Kuwajengea uwezo watumishi mbali mbali kuhusiana na mageuzi ya fedha za umma.

**Programu ya Kuwezesha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar kwa Wote**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata fursa ya kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya na wanapata haki ya msingi ya huduma za afya ikiwa ni msingi wa ustawi wa kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka 2026/2027, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 350.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya upembuzi yakinifu kuhusu kuanzishwa kwa mfuko wa usawa wa afya Zanzibar;
ii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa mradi kwa upande wa Unguja na Pemba;
iii. Kusaidia huduma za kiutawal na uratibu wa mfuko wa usawa wa afya; na
iv. Kuhamasisha na kupata rasilimali za kifedha kwa ajili ya bima ya afya ya pamoja kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**Programu ya Msaada wa Kiufundi kwa ajili ya Kukuza Uwezo wa Uhamasishaji na Utafutaji Rasilimali Fedha**

Programu ina Lengo la kuimarisha uwezo wa kitaasisi na kiufundi katika uhamasishaji, usimamizi na uendelevu wa rasilimali fedha kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka 2026/2027, Mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 4.77 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Ziliopangwa Kutekelezwa***

i. Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali fedha za mabadiliko ya tabianchi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;
ii. Kuwajengea uwezo wasimamizi wa mradi wa Bima ya Afya katika utekelezaji bora wa bima ya afya kwa wote ikijumuisha usimamizi wa fedha, mifumo ya bima na mifumo ya malipo; na
iii. Kutoa mafunzo kwa watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango juu ya usimamizi wa Fedha.

### 5.10.1 Tume ya Mipango Zanzibar

Tume ya Mipango ina jukumu la kuandaa, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya muda mfupi, wa kati na mrefu ya taifa, pamoja na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar na mikakati yake ya utekelezaji. Aidha, Tume husimamia uratibu na ulinganifu wa mipango ya sekta zote ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za Taifa, hufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ili kuhakikisha thamani ya fedha inafikiwa, na huimarisha mifumo ya takwimu na taarifa kwa ajili ya maamuzi ya kisera na kiutawala. Pia, Tume huratibu masuala ya maendeleo endelevu, kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu sera za kiuchumi, kijamii na kimazingira, kuratibu ushirikiano wa maendeleo na washirika wa kimataifa, na kukuza matumizi ya tafiti na ushahidi katika kupanga na kutekeleza maendeleo ya taifa.

Kwa mwaka 2026/2027, Tume ya Mipango imepangiwa jumla ya TZS 29.02 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza programu moja na miradi mitatu ya maendeleo.

**Programu ya Uratibu wa Mikakati ya Ukuaji Shirikishi**

Programu ina lengo la kuhakikisha ukuaji wa kiuchumi unaonufaisha makundi yote ya jamii kwa kuimarisha ushirikiano wa wadau, kuratibu mikakati ya maendeleo na kufuatilia utekelezaji wake. Programu hii inalenga kuinua hali ya kipato cha mwananchi kwa kuanzisha jukwaa la kitaifa la wafanyabiashara

wadogo wadogo na wa kati (MSME), kufanya utafiti wa kina wa umasikini katika maeneo yaliyoainishwa katika ripoti ya Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS 2024/25). Vilevile, inajumuisha kuimarisha utambuzi, upimaji na usajili wa ardhi ili kuongeza usalama wa umiliki na kuwezesha matumizi bora ya rasilimali ardhi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2026/2027, program hii imepangiwa kutumia TZS 9.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanzisha jukwaa la kitaifa la wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati (MSME);
ii. Kuhamasisha urasimishaji kwa wafanyabiashara wadogo, wakati na wakubwa (MSMEs) na ubunifu;
iii. Kufanya tafiti ndogo ndogo za kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia makundi hatarishi; na
iv. Kuratibu shughuli za utambuzi, upimaji na usajili wa ardhi.

***Mradi wa Uratibu na Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo***

Mradi una lengo la kuratibu shughuli za upangaji na usimamizi wa rasilimali fedha zinazotengwa na kutolewa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Mradi pia una lengo la kuimarisha uwezo wa Wizara na Taasisi za Serikali ili ziweze kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ufanisi kwa kuweka mifumo ya uwazi na jumuishi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa TZS 14. 90 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati (ZADEP) wa 2026- 2031;
ii. Kuwajengea uwezo wadau wakiwemo watendaji wa Wizara/Taasisi za Serikali juu Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati (ZADEP) wa 2026-2031;

iii. Kuandaa Mpango wa Utekelezaji, Mkakati wa Mawasiliano na Mkakati wa Utafutaji wa Rasilimali Fedha kwa Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati (ZADEP) wa 2026- 2031;
iv. Kuandaa Mwelekeo wa Muda Mrefu wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050;
v. Kuratibu zoezi la uthamini na uhakiki wa mali za wananchi wanaopisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
vi. Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya uendelezaji wa Mfumo Jumuishi wa Uratibu wa Mipango ya Maendeleo (ZiPS) pamoja na kuunganisha Mfumo huo na mifumo mengine inayohusiana na miradi ya maendeleo; na
vii. Kuratibu zoezi la uandaaji wa upembuzi yakinifu kwa programu na miradi ya maendeleo.

***Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa***

Mradi huu unalengo la kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mipango, Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2026-2031, Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030. Mradi unahusisha utekelezaji wa mifumo ya kufuatilia na kupima maendeleo ya miradi ya maendeleo ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa vigezo vilivyowekwa. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa TZS 2.42 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuandaa Nyenzo ya Ufuatiliaji na Tathmini (M&E framwork) wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2026-2031;
ii. Kushiriki katika mikutano na majukwaa ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ya Mipango ya Maendeleo na Malengo ya Maendeleo Endelevu;
iii. Kufanya mapitio ya Dira ya Maendeleo Zanzibar 2050;
iv. Kufanya tathmini ya programu na miradi ya maendeleo;

v. Kuwajengea uwezo Maafisa wa Ufuatiliaji na Tathmini kutoka MDAs, Taasisi zinazojitegemea, LGAs na NSA;
vi. Kuandaa na kuchapisha ripoti ya utekelezaji ya mwaka 2026/2027;
vii. Kuandaa na kuchapisha Ripoti ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2026/2027; na
viii. Kuwajengea uwezo wadau juu ya Sera ya Ufatiliaji na Tathmini ya Zanzibar 2026.

***Mradi wa Kuendeleza Tafiti za Kimkakati***

Mradi una lenga kukuza uwezo wa kitaasisi na kitaalamu katika kufanya tafiti zenye mwelekeo wa kimkakati, ambazo zitasaidia kutoa mapendekezo ya kisera, kubaini maeneo ya vipaumbele vya maendeleo na kusaidia katika uundaji wa mipango inayozingatia ushahidi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 2.20 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha Ajenda ya Taifa ya Utafiti, Sera ya Utafiti;
ii. Kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Ajenda Mpya ya Utafiti ya Zanzibar (2026–2031);
iii. Kufanya tafiti nne (4) za kimkakati na kuimarisha masuala ya ubunifu katika maeneo ya kiuchumi na kijamii ikiwemo zao la karafuu, uzalishaji wa chumvi na sekta miliki (real estate) na teknolojia.
iv. Kuanzisha na kuunganisha mfumo wa kuhifadhi tafiti kwa kushirikiana na Taasisi za utafiti Zanzibar;
v. Kuandaa mpango wa utekelezaji wa uchumi wa kidigital kwa Zanzibar na kuandaa muhtasari wa Sera; na
vi. Kuanzisha mfumo wa takwimu za kiuchumi Zanzibar.

### 5.10.2 Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ni Taasisi yenye jukumu la msingi la kukusanya, kuchambua na kutoa takwimu rasmi za Taifa zinazotumika katika

kupanga, kutekeleza na kufuatilia mipango ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, na sekta nyingine muhimu za maendeleo ya Taifa ili kusaidia maamuzi ya kisera na kiutawala yanayotokana na ushahidi. Afisi inatekeleza programu moja (1) na mradi mmoja (1), kwa mwaka 2026/2027 imepangiwa jumla ya TZS 8.52 bilioni (TZS 1.86 bilioni kutoka Serikalini na TZS 6.65 bilioni Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP-II)**

Programu ina lengo la kuimarisha shughuli za kitakwimu Zanzibar kwa kuwezesha ukusanyaji, upatikanaji na utoaji wa takwimu za kawaida (routine data) kwa wakati. Programu hii itawezesha uzalishaji na usimamizi wa takwimu, uimarishaji wa mifumo ya kitakwimu na miundombinu, maendeleo ya rasilimali watu kwa Taasisi za Serikali kupitia Mfumo wa Takwimu Zanzibar ili kusaidia uimarishaji na upatikanaji wa takwimu rasmi. Kwa mwaka 2026/2027, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 6.40 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Uchapishaji wa matoleo rasmi ya takwimu kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya matumizi ya mipango na maamuzi ya kisera;
ii. Kufanya Utafiti wa Ufuatiliaji wa Kaya (National Panel Survey – NPS) kwa lengo la kufuatilia mabadiliko ya kijamii na kiuchumi;
iii. Kufanya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi kwa mwaka 2026/2027 ili kupata takwimu za nguvu kazi na ajira;
iv. Kufanya Utafiti wa Sekta isiyo Rasmi kwa mwaka 2026 ili kubaini mchango wake katika uchumi wa Taifa;
v. Kufanya Sensa ya Viwanda ya Mwaka na Robo Mwaka kuhusu uzalishaji mali viwandani ili kupima mwenendo wa sekta ya viwanda;
vi. Kufanya Utafiti wa Ajira na Mapato kwa mwaka 2025/2026 ili kubaini hali ya ajira na viwango vya mapato;
vii. Kufanya Utafiti wa Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2025 kwa lengo la kuboresha takwimu za uzalishaji na tija;

viii. Kuwajengea uwezo watakwimu na watendaji katika Mfumo wa Takwimu Zanzibar ili kuongeza ufanisi na ubora wa takwimu; na

ix. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za mradi kwa kuhakikisha ufanisi na uwajibikaji.

***Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia***

Mradi una lengo la kuimarisha uzalishaji na matumizi ya takwimu za jinsia ambazo husaidia katika kubuni sera na mipango ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa ambayo inazingatia mahitaji na haki za jinsia hasa katika masuala ya elimu, afya, ajira na haki za kijamii. Vile vile, kutoa elimu ya dhana ya udhalilishaji wa kijinsia na aina zake, kutambua makundi au maeneo ambayo yako katika hatari zaidi ya udhalilishaji wa kijinsia. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.11 bilioni (TZS 1.86 bilioni kutoka Serikalini na TZS 250.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Serikali***

i. Kufanya vikao vya uhamasishaji kati ya mtumiaji na mzalishaji wa takwimu za jinsia;

ii. Kufanya mafunzo ya dhana na tafsiri ya jinsia;

iii. Kuboresha mfumo wa watumiaji wa takwimu za kijinsia;

iv. Kufanya ziara za masomo ya muda mfupi kuhusiana na masuala ya takwimu za kijinsia;

v. Kutoa matoleo ya takwimu za udhalilishaji wa kijinsia kila mwezi;

vi. Kuandaa mpango mkakati wa takwimu za kijinsia wa Zanzibar; na

vii. Uratibu wa shughuli za takwimu za jinsia.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Washirika wa Maendeleo***

i Kuandaa mfumo wa kidigitali wa ukusanyaji na usimamizi wa takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; na

ii Kutoa mafunzo ya mfumo kwa wadau wanaotumia takwimu za kijinsia.

## 5.11 Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo

Wizara ina jukumu la kuendeleza sekta ya habari, sanaa, utamaduni na michezo nchini kwa kusimamia taarifa kupitia magazeti, redio na televisheni, kuendeleza utamaduni na urithi wa Taifa, pamoja na kukuza sanaa na ubunifu kwa ajili ya ajira na maendeleo ya kiuchumi. Aidha, Wizara inahusika na kuimarisha michezo kwa kukuza vipaji, kuboresha miundombinu na kuhakikisha ushiriki katika mashindano ya Kitaifa na Kimataifa, ambapo moja ya mashindano makubwa kwa Taifa ni AFCON. Ushiriki wa timu ya Taifa katika AFCON ni kielelezo cha jitihada za Serikali katika kukuza michezo na kuimarisha mshikamano wa Kitaifa. Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu moja (1) na mradi mmoja (1) utakaogharimu TZS 219.90 bilioni kutoka Serikali.

### Programu ya Kuimarisha na Kuendeleza Viwanja vya Michezo

Programu hii inalenga kuiwezesha sekta ya michezo kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo itakayokidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa, pamoja na kuimarisha afya ya jamii kupitia ushiriki wa michezo na mazoezi ya mwili. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 204.90 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na ujenzi wa Mji wa Michezo - Fumba; na
ii. Kuendelea na ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya na Mkoa.

### Mradi wa Ujenzi wa Kijiji cha Utamaduni na Kituo cha Ubunifu wa Kazi za Sanaa Bweleo

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuwa na kivutio mama cha kuhifadhi, kulinda, kuendeleza na kurithisha amali, ujuzi, maadili, lugha, sanaa na fani zote za utamaduni ili kuendeleza mila, silka, desturi na maadili ya Wazanzibari. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa Chuo cha Utamaduni na Sanaa; na
ii. Ununuzi wa vifaa vya Afisi kwa ajili ya Chuo cha Utamadumi.

## 5.12 Wizara ya Kazi na Uwekezaji

Wizara ina jukumu la kusimamia Sera, Sheria, kanuni za ajira, mahusiano ya kikazi, kukuza ajira za staha pamoja na kutatua migogoro kwa waajiri na waajiriwa. Aidha, inahamasisha na kurahisisha uwekezaji wa ndani na nje ya nchi kupitia maboresho ya sera rafiki, kupunguza vikwazo vya kiutawala na taratibu za uwekezaji ili kuongeza ufanisi, ushindani na tija ya kiuchumi. Kuimarisha uwekezaji katika visiwa, maeneo huru ya kiuchumi na uchumi wa buluu kwa matumizi endelevu ya rasilimali za bahari. Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu moja (1) ya maendeleo itakayogharimu TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini.

### Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kukuza maeneo huru ya uwekezaji kupitia uimarishaji wa miundombinu ya barabara, maji, umeme na mawasiliano katika maeneo yaliyoainishwa kwa uwekezaji, ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2026/2027, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kusambaza miundombinu ya barabara katika eneo la uwekezaji Fumba; na
ii. Ujenzi wa maghala ya Uwekezaji katika maeneo ya Viwanda Amani.

## 5.13 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

Wizara ina jukumu la kuendeleza sekta za kilimo na mifugo ambazo ni muhimu katika kukuza uchumi kupitia kuongeza uzalishaji, kuwa na uhakika wa chakula, kutoa ajira kwa wananchi. Aidha, kuimarisha akiba ya chakula, kuboresha miundombinu ya mifugo, kuendeleza tafiti za kilimo na mifugo, kuimarisha mashamba ya viungo na bustani za mimea. Kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo na utoaji wa mafunzo kwa wakulima na wafugaji ili kuongeza tija na ufanisi wa uzalishaji.

Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu tatu (3) na mradi mmoja (1) itakayogharimu jumla ya TZS 145.00 bilioni (TZS 86.55 bilioni kutoka Serikalini na TZS 58.46 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

### Programu ya Maendeleo ya Kilimo

Programu ina lengo la kusimamia sekta za kilimo kwa kuongeza upatikanaji wa mazao ya kilimo yaliyosalama, upatikanaji wa chakula katika ngazi ya Kitaifa pamoja na kuwajengea uwezo wakulima juu ya mifumo ya chakula. Kwa mwaka 2026/2027, programu inatarajia kutekeleza mradi minne (4) ya Maendeleo.

### *Mradi wa Kuimaarisha Kiwango Bora cha Akiba ya Chakula*

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuimaarisha kiwango bora cha akiba ya chakula kimkakati ili kushughulikia uhaba wa chakula nchini na kukabiliana na mahitaji ya dharura katika ngazi ya Kaya na Taifa. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 75.50 bilioni kutoka Serikalini.

### *Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi chakula Mangapwani-Unguja na Chamanangwe-Pemba (Silos Complex);
ii. Ukarabati wa maghala 11 Unguja na Pemba; na
iii. Ununuzi wa chakula cha akiba.

***Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa Kukuza Uchumi Jumuishi***

Mradi una lengo la kubadili mifumo ya chakula ili kuchochea uchumi jumuishi, kuongeza usalama wa chakula na lishe nchini pamoja na kuimarisha minyororo ya thamani ya mazao ya chakula ikiwemo: migomba, mihogo na mwani kwa kutumia mbinu jumuishi zinazokabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuongeza ujuzi na uwezo wa vijana na wanawake waweze kujiajiri na kupata fursa za kilimo katika miradi ya kijamii. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 4.63 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanzisha mashamba 20 ya mfano ya uzalishaji wa zao la muhogo na 20 ya kilimo mchanganyiko cha mwani pamoja na ufugaji wa majongoo bahari katika eneo moja;
ii. Kusaidia upatikanaji wa mbegu bora za mwani;
iii. Kuwajengea uwezo wakulima 300 katika kilimo bora cha muhogo;
iv. Kutoa huduma za kuanzisha biashara kwa wanawake na vijana 700 katika biashara za kilimo na uongezaji thamani katika zao la mwani, majongoo bahari, muhogo na ndizi;
v. Kuanzisha vituo viwili vya huduma za malezi pamoja na utoaji wa vifaa vinavyopunguza mzigo wa malezi ili kuboresha upatikanaji wa huduma za malezi kwa wanawake na vijana; na
vi. Kuimarisha miundombinu na kuwapa vifaa vikundi sita (6) vya mwani katika masuala ya usarifu, kufungasha na kuongeza thamani ili kuongeza ushidani wa kibiashara.

***Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejeshaji wa Ardhi***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la uendelezaji wa mifumo ya chakula, matumizi endelevu ya ardhi na urejeshaji wa uoto wa asili katika maeneo yaliyoathirika pamoja na uhifadhi wa misitu na kusimamia rasilimali hiyo. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2026/2027, umepangiwa jumla ya TZS 841.73 milioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kusimamia eneo la ardhi la Kaskazini-Unguja na rasilimali zake kwa namna ya kuunganisha maslahi ya watu na mazingira;
ii. Uhifadhi na ukarabati wa makaazi ya asili kwa kulinda, kusimamia na kurejesha maeneo ya asili; na
iii. Kuandaa mipango ya usimamizi na matumizi bora ya ardhi na maji kwa ngazi ya shehia na vijiji na kuwapatia mafunzo juu ya mipango husika.

***Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kusaidia uhimilivu wa mfumo wa chakula kwa kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, kupitisha teknolojia za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kujenga uwezo wa uhimilivu katika mifumo ya chakula. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 39.71 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ukarabati wa majengo ya maabara za Taasisi ya Utafiti wa Mifugo - Kizimbani Unguja;
ii. Kuendeleza tafiti za kupata mbegu bora zinazoweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi;
iii. Kuanza ukarabati wa vituo vya huduma kwa wakulima na miundombinu ya uzalishaji wa mbegu;
iv. Kufundisha maafisa ugani kuhusiana namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari;
v. Kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu bora za uzalishaji, na teknolojia ya kilimo shadidi;
vi. Kuanza ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde 10 ya Bumbwisudi, Mtwango, Kianga, Kibokwa na Mwera kwa Unguja, Makombeni, Tibirinzi, Weni, Saninga na Kinyakuzi kwa Pemba; na

vii. Kuwafundisha vijana kutoa huduma mashambani kwa kutumia trekta ndogo ndogo za kilimo.

**Programu ya Maendeleo ya Mifugo**

Programu ina lengo la kuimarisha na kuinua sekta ya mifugo kwa wafugaji wadogo wadogo, kudhibiti maradhi ya mifugo na kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao yake. Kwa mwaka 2026/2027, Programu inatarajia kutekeleza miradi mitatu (3).

***Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuendeleza miundombinu ya mifugo kwa kutoa huduma bora kwa jamii za wafugaji na wakulima, kuimarisha na kuongeza ufanisi katika vituo vya vizuizi vya mifugo. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.50 bilioni kutoka Serikalini.

**Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa**

i. Ukarabati wa miundombinu ya karantini Kisakasaka na Donge Muanda, kwa Unguja na Nziwengi – Gando-Pemba;
ii. Ununuzi wa mitambo ya kuzalisha gesi ya 'Liquid Nitrogen';
iii. Ujenzi wa vituo vya kisasa vya matibabu ya mifugo na ushauri wa kitaalamu katika kila Wilaya;
iv. Kudhibiti wanyama waharibifu wa mazao ya kilimo na mifugo;
v. Kuzindua na kuimarisha maudhui ya kilimo TV; na
vi. Uimarishaji wa kituo cha kupandishia ng'ombe kwa njia ya sindano.

***Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa Kuongeza Tija na Uzalishaji Kupitia Huduma za Kisasa za Kilimo katika Umwagiliaji***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuchangia uimarishaji, uhakika wa chakula na kuongeza kiwango cha kipato kwa wakulima wa mpunga Zanzibar, pamoja na kuongeza tija ya mpunga katika mashamba ya umwagiliaji. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.47 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukamilisha ujenzi wa maghala na hifadhi katika skimu sita (6) za umwagiliaji;
ii. Kuwajengea uwezo wakulima na maafisa ugani;
iii. Ununuzi wa vifaa vya ziada vya usimamizi wa maji (vifaa vya kupimia kiwango cha maji, vifaa vya kupimia pH) kwenye maeneo ya mradi; na
iv. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mradi.

***Mradi wa Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa Wafugaji Wadogo Unaozingatia Mabadiliko ya Tabianchi***

Mradi una lengo la kuchangia mabadiliko katika mnyororo wa thamani wa maziwa ili kuboresha maisha ya watu, kuongeza uhakika wa chakula, na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2026/2027, umepangiwa jumla ya TZS 7.80 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Utoaji wa ng’ombe wa maziwa na msaada wa ujenzi wa mabanda ya ng’ombe kwa kaya zilizo katika mazingira magumu;
ii. Kujenga uwezo kwa wakulima wadogo kupitia skuli za wakulima wa mifugo;
iii. Kutoa msaada wa huduma za ugani na huduma za afya ya mifugo;
iv. Kuunda na kuimarisha vikundi vya wazalishaji wa maziwa na vyama vya ushirika;
v. Uanzishaji na ukarabati wa vituo vya kukusanyia maziwa;
vi. Usimamizi na ufuatiliaji wa mradi; na
vii. Uhamasishaji wa matumizi ya nishati bora na nishati jadidifu kwa ajili ya kupoza maziwa na usindikaji mdogo wa maziwa.

**Programu ya Maendeleo ya Tafiti za Kilimo na Mifugo**

Programu ina lengo la kuimarisha miundombinu na uwezo wa utafiti wa kilimo na mifugo katika maabara za Unguja na Pemba, shamba la viungo na uanzishwaji wa bustani ya mimea. Kwa mwaka 2026/2027, programu inatarajia kutekeleza miradi miwili (2).

***Mradi wa Kuimarisha Shamba la Viungo na Bustani ya Mimea***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha utendaji na uzalishaji wa Shamba la viungo la Kizimbani na kuanzisha bustani ya mimea itakayosaidia utafiti wa kilimo, uhifadhi wa mimea, elimu kwa umma na utalii endelevu chini ya usimamizi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 5.55 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Uanzishwaji wa mashamba darasa kwa mazao ya viungo, mimea tiba na aina ya viumbe hai adimu;
ii. Ujenzi wa kituo cha taarifa na nyaraka kwa ajili ya aina za viumbe hai za mimea na elimu kwa wageni;
iii. Kuhifadhi na kuboresha miundombinu ya utafiti wa kilimo;
iv. Uchimbaji wa kisima kirefu na uwekaji wa miundombinu ya kuhifadhi maji na umwagiliaji; na
v. Uanzishwaji wa vivutio vya kiutalii kwa watalii wa ndani na nje.

***Mradi wa Kuimarisha Miundombinu na Uwezo wa Utafiti wa Kilimo, Maliasili na Mifugo***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha uwezo wa kufanya utafiti wa kilimo, maliasili na mifugo, kupitia uanzishaji wa maabara za utafiti, vituo vya utafiti na majaribio ya Wanyama pamoja na kituo madhubuti cha uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka kwa taarifa za utafiti wa kilimo, maliasili na mifugo. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa maabara kuu za utafiti Chamanagwe - Pemba; na
ii. Ujenzi wa mabanda ya utafiti wa kuku, sungura na mbuzi katika kituo cha utafiti wa mifugo Chamanangwe - Pemba.

***Mradi wa Ulinzi wa Misitu ya Mwambao wa Zanzibar kwa Manufaa Mchanganyiko***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kulinda makaazi ya nchi kavu na ya pwani ya Zanzibar kwa manufaa mbali mbali kwa kutumia mbinu ya usimamizi wa kimandhari. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.99 bilioni.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya mapitio ya kina ya sera na kanuni zilizopo (Misitu, Mazingira na Uchumi wa Buluu);
ii. Kufanya mashauriano na wadau Unguja na Pemba kuhusu mapungufu ya sera na changamoto za utekelezaji na usimamizi;
iii. Kufanya tathmini ya hali ya utekelezaji na usimamizi shirikishi wa misitu;
iv. Kufanya mapitio na uidhinishaji wa miongozo ya usimamizi shirikishi wa misitu;
v. Kutoa mafunzo na usaidizi wa kitaalamu katika uhifadhi wa mazingira na misitu; na
vi. Kuimarisha uwezo jumuishi wa kijinsia katika usimamizi wa misitu ya jamii.

## 5.14 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Wizara imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha ustawi wa jamii kupitia upatikanaji wa huduma bora kwa jamii, wazee na watoto. Miongoni mwa majukumu yake ni kuhudumia na kulinda wazee na watoto, kutokomeza ukatili na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wa kike, pamoja na kuimarisha na kukuza usawa wa kijinsia nchini.

Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza miradi minne (4) itakayogharimu jumla ya TZS 16.90 bilioni (TZS 7.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 9.90 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Mradi wa Hifadhi ya Wazee***

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kukuza ustawi wa wazee kwa kuimarisha usalama wao, kuhakikisha wanaishi katika makaazi mazuri na wanapata huduma za msingi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na ukarabati wa makaazi ya wazee Sebleni na Limbani; na
ii. Ununuzi wa vifaa na samani kwa makaazi ya wazee.

***Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Kulelea Watoto***

Mradi una lengo la kutoa makaazi salama, yenye heshima na yanayokidhi mahitaji ya msingi kwa watoto waliopoteza wazazi au walezi, kupitia ushirikiano wa wadau mbalimbali. Mradi unakusudia kuboresha ustawi wa watoto yatima, kuwawezesha kisaikolojia, kijamii na kuwaandaa kuwa raia wenye mchango chanya katika jamii. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza na ujenzi wa kituo cha kulelea Watoto Unguja.

***Mradi wa Kutokomeza Uzalilishaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana***

Mradi una lengo la kuimarisha haki za wanawake na wasichana kwa kupambana na ukatili wa kijinsia sambamba na uhamasishaji wa haki za binaadamu. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 636.32 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kutafsiri kwa lugha ya kiswahili Mpango wa Kutokomeza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji;
ii. Kuandaa mikutano ya vikundi kazi kwa ajili ya kupambana vitendo vya udhalilishaji;
iii. Ununuzi wa vifaa vya Afisi;
iv. Kuratibu utekelezaji wa mradi;
v. Kufanya mafunzo kwa maafisa juu ya modeli mpya (Modeli Sasa) ili kuweza kutumika katika kufanya mikutano ya kampeni ya kijamii; na
vi. Kutathmini mbinu za kijamii katika kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

***Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja)***

Mradi una lengo la kukuza fursa za kiuchumi kwa wanawake pamoja na kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji Tanzania. Kwa mwaka 2026/2029, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 9.26 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuwajengea uwezo wanawake juu ya stadi za maisha na biashara;
ii. Kufanya mafunzo kwa vikundi vya wanawake au binafsi kwenye mpango wa biashara;
iii. Kutambua vikundi vya jamii kwa ajili ya majukwaa ya wajasiriamali wanawake ili kuwawezesha kiuchumi;
iv. Kutathmini masoko na mifumo ya biashara;
v. Ununuzi wa vifaa vya kufunzia kwa makundi yaliotambuliwa;
vi. Kufanya tafiti ya kuelewa hali ya desturi za kijamii na tabia hasi za usawa wa kijinsia na ukatili wa udhalilishaji;
vii. Kufanya ziara ya kimafunzo Rwanda kwa kujifunza 'Bandebehero model';
viii. Kujenga na kununua vifaa vya jengo la huduma za kisaikolojia na nyumba salama;

ix. Kukuza fursa za kiuchumi kwa wanawake kupitia mifumo ya kijamii;
x. Ubunifu na ushirikishwaji;
xi. Usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya mradi; na
xii. Kuimarisha huduma za kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

## 5.15 Wizara ya Maji, Nishati na Madini

Wizara inasimamia sekta kuu tatu maji, nishati na madini ambazo ni nguzo muhimu katika kuchochea maendeleo ya taifa na kuboresha ustawi kwa jamii. Wizara inalenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za maji safi na salama, kuimarisha upatikanaji wa nishati ya uhakika na nafuu, pamoja na kusimamia matumizi bora ya rasilimali madini kwa ajili ya kukuza uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu mbili (2) na mradi mmoja (1) itakayogharimu jumla ya TZS 458.82 bilioni (TZS 315.42 bilioni kutoka Serikalini na TZS 143.40 bilioni kwa Washirika wa Maendeleo).

**Program ya Kuimarisha Mifumo ya Maji Zanzibar**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha uwepo wa mifumo madhubuti na imara ya usambazaji wa maji safi na salama pamoja na kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa maji taka sambamba na upatikanaji endelevu wa maji safi na salama katika maeneo ya Mijini na Vijijini kwa Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2026/2027, programu hii itatekelezwa kupitia miradi kumi na mbili (12) ya maendeleo kama ifuatavyo:

***Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Maji kwa Mikoa ya Unguja***

Mradi huu una lengo la kuhakikisha miundombinu ya usambazaji wa maji safi na salama katika Mikoa yote ya Unguja ina kuwa imara na kuweza kuhakikisha upatikajani wa huduma hiyo Mijini na Vijijini. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS 35.55 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Uimarishaji wa huduma za maji Mkoa wa Magharibi;
ii. Uimarishaji wa huduma za maji Mkoa wa Kusini Unguja; na
iii. Uimarishaji wa miundonbinu ya maji Kaskazini Unguja.

***Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar***

Mradi huu unalenga kuboresha miundombinu ya maji, kuongeza ufanisi wa usambazaji na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa rasilimali za maji ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 13.90 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kumlipa Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi za usimamizi wa mradi; na
ii. Kumlipa Mkandarasi kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa miundombinu ya Maji

***Mradi wa Kuimarisha Usalama wa Maji Zanzibar***

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya mjini na vijijini Unguja na Pemba. Mradi unatarajia kuijengea uwezo sekta ya maji juu ya usimamiaji wa usalama na upatikanaji wa maji nchini kwa kuanda mikakati na miongozo ya mageuzi, kuanzisha mfumo jumuishi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira sambamba na kutoa mafunzo ya usimamiaji wa rasilimali maji pamoja na uimarishaji wa huduma za uendeshaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar. Kwa mwaka 2026/2027. Mradi huu umepangiwa jumla ya 9.61 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kuandaa mkakati na muongozo wa usimamizi wa maji;
ii. Kuanzisha mifumo jumuishi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira;

iii. Kuwajengea uwezo watendaji wa Wizara na Taasisi zake;
iv. Malipo kwa Washauri Elekezi wa kazi mbalimbali ikiwemo utayarishaji wa michoro na ramani, usanifu wa mradi na mchanganuo wa gharama; na
v. Uendeshaji wa mradi.

***Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi***

Mradi huu unalenga kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi kwa wakaazi wa eneo la Mjini Magharib kupitia uendelezaji wa miundombinu ya kisasa ya usambazaji maji kwa kubadilisha na kupanua mtandao wa usambazaji wa maji ili kuongeza uwezo wa upatikanaji na kupunguza upotevu wa maji. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 25.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kumlipa Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi za usimamizi wa mradi; na
ii. Kumlipa Mkandarasi kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa miundombinu ya Maji.

***Mradi wa Usimamizi na Uangalizi Bora wa Rasilimali Maji***

Mradi unalenga kuimarisha usimamizi na uendelevu wa rasilimali maji kwa kutambua na kusajili visima binafsi, kuboresha ubora wa maji kupitia matibabu stahiki, na kulinda vyanzo vya maji dhidi ya uharibifu. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 30.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kujengea uwezo na kusajili Jumuiya za uhifadhi wa vyanzo vya maji katika ngazi ya Shehia;
ii. Kuanzisha Jumuiya mpya za uhifadhi wa vyanzo vya maji katika ngazi ya Shehia za Mkoa Mjini Magharibi;
iii. Mafunzo kwa wafanyakazi juu ya ubora wa maji na kufanya uchambuzi wa maji taka;

iv. Ununuzi wa vifaa vya ufuatiliaji wa ubora wa maji; na
v. Kuandaa muongozo wa ujenzi wa miundombinu ya maji safi na maji taka.

***Mradi wa Uandaaji wa Mpango Mkuu wa Rasilimali Maji, Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira***

Mradi huu unalenga kuandaa Mpango Mkuu wa Maji na Usafi wa Mazingira kwa Unguja na Pemba ili kuboresha upangaji, usimamizi na uendelezaji endelevu wa rasilimali maji, pamoja na huduma za usambazaji na usafi wa mazingira. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 840.74 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanda Mpango Mkuu wa Usambazaji Maji, Rasimali Maji na Usafi wa Mazingira-Unguja na Pemba; na
ii. Kuwajengea uwezo watendaji wa Wizara juu ya usimamizi wa rasilimali maji.

***Mradi wa Kuimarisha Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Awamu ya II)***

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za maji safi, usimamizi endelevu wa maji taka katika visiwa vya Zanzibar na kuimarisha uwezo wa Taasisi katika kusimamia rasilimali za maji kwa ufanisi na endelevu. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuajiri Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi za utayarishaji michoro na ramani, usanifu wa mradi, mchanganuo wa gharama pamoja na uandaji wa nyaraka za zabuni za ununuzi kwa Mkandarasi katika kazi;
ii. Kufanya utafiti wa msingi kuhusu upatikanaji wa huduma za maji taka;
iii. Kupitia na kuandaa rasimu ya sheria za maji safi na usafi wa mazingira 2006 pamoja na kanuni zake; na

iv. Ununuzi wa vifaa vya kisasa vya uchunguzi na ufatiliaji wa maji ya chini ya ardhi na miundombinu ya usambazaji maji.

***Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji***

Mradi unalenga kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi kupitia ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika skimu husika. Mradi utasaidia kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji, kupunguza upotevu wa maji pamoja na kuboresha afya na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 50.20 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kujenga na kukarabati miundombinu ya maji katika skimu tisa (9) Pandani, Ole, Muambe – Kengeja, Madenjani, Wingwi, Chokocho, Sizini, Chambani na Wawi;
ii. Kufunga mabomba na vifaa vya usambazaji wa maji; na
iii. Kufanya ufuatiliaji na matengenezo ya mfumo wa maji.

***Mradi wa Udhibiti, Ugavi na Matumizi Endelevu ya Nishati ya Umeme***

Mradi unalenga kuboresha udhibiti, ugavi na matumizi endelevu ya nishati ya umeme kwa kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika, salama na wenye gharama nafuu kwa jamii. Mradi utajikita katika kuimarisha miundombinu ya umeme, matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira, pamoja na kuhamasisha matumizi bora ya nishati ili kupunguza upotevu wa umeme na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 9.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuboresha na kusambaza miundombinu ya umeme;
ii. Kufunga vifaa vya matumizi bora ya nishati na teknolojia rafiki kwa mazingira; na
iii. Kutoa mafunzo kwa wataalamu wa sekta ya nishati.

*Mradi wa Ujenzi wa Matangi*

Mradi unalenga kuongeza uwezo wa uhifadhi na usambazaji wa maji safi kwa wananchi. Mradi huu utasaidia kuhakikisha upatikanaji wa maji ya uhakika, kupunguza changamoto za upungufu wa maji pamoja na kuboresha huduma za kijamii na afya. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 5.13 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kujenga matangi 10 ya kuhifadhi maji; na
ii. Kufunga mifumo ya mabomba ya kuingiza na kusambaza maji.

*Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji Maji Safi katika Mji wa Michezo*

Mradi unalenga kuboresha huduma ya maji safi na salama kwa wakaazi wa eneo hilo kupitia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usambazaji wa maji. Mradi utasaidia kuongeza upatikanaji wa maji ya uhakika, kupunguza upotevu wa maji pamoja na kusaidia maendeleo ya makaazi, huduma za kijamii na shughuli za kiuchumi katika Mji wa Michezo. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 19.20 bilioni kutoka Serikalini.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kujenga na kukarabati miundombinu ya usambazaji maji safi;
ii. Kufunga mabomba na vifaa vya kusambaza maji kwa wananchi; na
iii. Kujenga vituo vya kuhifadhi na kusambaza maji.

*Mradi wa Uwekaji wa Mifumo ya Usafirishaji wa Maji Taka katika Mji wa Michezo- Fumba*

Mradi una lengo la kuboresha usafi wa mazingira na huduma za maji taka kupitia uwekaji wa mifumo bora ya ukusanyaji na usafirishaji wa maji taka katika eneo la Mji wa Michezo uliopo Fumba. Mradi utasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira, kuimarisha afya ya jamii pamoja na kusaidia maendeleo endelevu ya

makaazi na miundombinu ya kisasa. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 6.29 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kujenga na kufunga mifumo ya mabomba ya maji taka;
ii. Kujenga vituo vya kukusanyia na kusambaza maji taka; na
iii. Kufanya ukaguzi na majaribio ya mfumo wa maji taka.

**Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar**

Programu ina lengo la kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma ya uhakika na endelevu ya nishati ya umeme katika maeneo yote ya Zanzibar. Program inatarajia kuimarisha mifumo na miundombinu ya usambazaji wa umeme ili wananchi waweze kufaidika na huduma hiyo katika maeneo yote ya Mijini na vijijini kwa Unguja na Pemba. Program hii inatekelezwa kupitia miradi tisa (9) .

***Mradi wa Maboresho ya Mfumo wa Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme***

Mradi unalenga kuimarisha mfumo wa usafirishaji na usambazaji wa umeme katika kwa kuongeza uwezo wa miundombinu ya mtandao wa umeme, kuboresha usimamizi wa mfumo wa umeme pamoja na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wananchi. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuongeza uhakika wa upatikanaji wa umeme, kupunguza muda wa hitilafu za umeme na kupanua huduma katika maeneo mapya yanayohitaji kuunganishwa na mtandao wa umeme. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 41.72 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Uwekaji wa waya chini ya ardhi katika eneo la Mji wa Michezo- Fumba;
ii. Kujenga na kufanya maboresho ya njia kuu za umeme za mkondo wa 33kV zenye urefu wa kilomita 320 kutoka kituo cha Wesha kuelekea Kaskazini na Kusini mwa Pemba;

iii. Kujenga njia mpya za umeme za mkondo wa 33kV kutoka Wesha hadi Gombani, Chanjaani, Zaire na Uwanja wa Ndege kwa kutumia nyaya za ardhini kwa urefu wa kilomita 80;
iv. Kujenga njia za kuunganisha mtandao wa umeme kwa mfumo wa "ring circuits" pamoja na kufikisha huduma katika maeneo mapya kwa urefu wa kilomita 115;
v. Kuweka mfumo wa mawasiliano wa "fiber optic" katika njia zote za umeme zitakazojengwa kwa jumla ya kilomita 320 ili kuimarisha mawasiliano na uendeshaji wa mfumo wa umeme;
vi. Kufunga mfumo wa "Distribution Management System (DMS)" pamoja na mfumo wa "Mini-SCADA" kwa ajili ya kusimamia mwenendo wa mtandao wa umeme katika Kisiwa cha Pemba;
vii. Kufunga vifaa vya kisasa vya udhibiti wa mtandao ikiwemo "auto-reclosers circuit breakers" katika maeneo 19 na "load break switches" maeneo 35;
viii. Kutoa mafunzo kwa watendaji wa Shirika la Umeme kuhusu matumizi, uendeshaji na matengenezo ya mifumo mipya ya kisasa itakayofungwa;
ix. Kununua trekta mbili zenye uwezo wa 250HP pamoja na krini za tani 10 kwa ajili ya kubeba nguzo na kufanya kazi za miundombinu ya umeme; na
x. Kununua gari tisa (9) yenye krini za tani 7 kila moja kwa ajili ya shughuli za ujenzi na matengenezo ya njia za umeme.

***Mradi wa Kuanzisha Vinu vya Kufua Umeme kwa Kutumia Majenereta***

Mradi unalenga kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika, salama na endelevu kwa kutafuta vyanzo mbadala vya uzalishaji wa umeme vitakavyosaidia kuongeza nguvu katika mfumo wa gridi ya umeme Zanzibar. Katika kufanikisha azma hiyo, Serikali imepanga kuanzisha kinu cha kuzalisha umeme chenye uwezo wa MW100 kwa Unguja na MW 34 kwa Pemba kwa kutumia majenereta ya kisasa. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 59.62 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i Kufanya upembuzi yakinifu na tathmini ya athari kwa mazingira na jamii;

ii Ununuzi na ufungaji wa majenereta ya kisasa ya kuzalisha umeme;

iii Ujenzi wa miundombinu ya vinu vya kuzalisha umeme;

iv Ujenzi wa mifumo ya kuhifadhia na kusambaza mafuta kwa ajili ya uendeshaji wa majenereta;

v Ujenzi wa vituo vya kupozea na kusambaza umeme;

vi Ufungaji wa mifumo ya udhibiti, uendeshaji na usimamizi wa mitambo; na

vii Kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani kupitia mafunzo maalumu ya uendeshaji na matengenezo ya mitambo hiyo.

***Mradi wa Ujenzi wa Kituo Kipya cha Kupozea Umeme***

Mradi unalenga kuimarisha mfumo wa uzalishaji na usambazaji wa umeme kupitia ujenzi wa kituo kipya cha kupozea na kuunganishia umeme katika eneo la Wesha. Kituo hicho kitapokea umeme unaozalishwa na majenereta yanayotumia mafuta ya HFO/LNG kwa lengo la kukuza nguvu ya umeme unaozalishwa na kuunganisha huduma hiyo katika mfumo wa usafirishaji wa umeme uliopo. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika, kuimarisha uthabiti wa huduma pamoja na kuongeza ufanisi wa mfumo wa usambazaji umeme Pemba. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 20.48 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizpangwa Kutekelezwa***

i. Kutengeneza miundombinu ya kuwezesha ujenzi wa kituo cha kukuza umeme;

ii. Kufunga transfoma mbili kwa ajili ya kukuza umeme kutoka 11kV kwenye 132kV; na

iii. Kuunganisha kituo cha uzalishaji umeme na mfumo wa gridi ya taifa yenye kiwango cha 132kV.

***Mradi wa Uwekaji wa Miundombinu ya Kuhifadhi na Kusafirisha Umeme***

Mradi unalenga kuanzisha na kuimarisha vyanzo mbadala vya uzalishaji wa umeme kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa nishati katika Gridi ya Taifa. Aidha, mradi unahusisha uwekaji wa miundombinu ya kuhifadhi umeme pamoja na ujenzi wa njia za kusafirishia umeme katika eneo la Bambi-Unguja. Utekelezaji wa mradi unatarajiwa kuongeza uthabiti wa huduma ya umeme, kupunguza upotevu wa nishati, pamoja na kuimarisha ufanisi wa mfumo wa usambazaji wa umeme. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 32.16 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kuhifadhi umeme;
ii. Ujenzi wa njia za kusafirishia umeme;
iii. Ujenzi wa kituo cha kupozea na kuunganishia umeme;
iv. Ufungaji wa mfumo wa usimamizi wa nishati na majaribio na kuingiza mfumo katika matumizi rasmi;
v. Kazi za ujenzi wa miundombinu ya ardhini; na
vi. Kufanya mafunzo ya kitaalamu pamoja na uhamishaji wa maarifa kwa watendaji husika.

***Mradi wa Uwekaji wa Miundombinu ya Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Nishati ya Jua katika Visima vya Maji***

Mradi unalenga kuweka miundombinu ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika visima 79 vya maji ambayo itasaidia kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji inayosababishwa na kukatika au kuzimika kwa umeme katika baadhi ya maeneo. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuongeza uhakika wa huduma ya maji, kupunguza gharama za matumizi ya nishati pamoja na kuimarisha matumizi ya nishati safi na endelevu. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 12.58 bilioni kutoka Serikalinio.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ununuzi na ufungaji wa paneli na pampu za umeme wa jua;
ii. Uwekaji wa mifumo ya udhibiti na uhifadhi wa nishati; na
iii. Ujenzi wa miundombinu ya usalama na majengo yanayohusiana na mradi;

***Mradi wa Kuimarisha Miundombinu na Uzalishaji wa Umeme***

Mradi unalenga kuzalisha umeme wa jua wenye uwezo wa 30 MW pamoja na kuweka mfumo wa kuhifadhi nishati ya umeme wenye uwezo wa 20MWh. Aidha, mradi unakusudia kuimarisha upatikanaji na uthabiti wa huduma ya umeme, kupunguza upotevu wa nishati katika mfumo wa usambazaji, pamoja na kuendeleza matumizi ya nishati safi na endelevu Zanzibar. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 31.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuzalisha umeme wa 30 MW kwa kutumia nishati ya jua;
ii. Kuweka mfumo wa kuhifadhi nishati ya umeme wenye uwezo wa 20MWh;
iii. Kujenga laini za usambazaji wa umeme za mkondo wa 33kV zenye urefu wa kilomita 210; na
iv. Kuweka mfumo wa utambuzi wa hitilafu katika miundombinu ya umeme.

***Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati Zanzibar***

Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo Taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati ili ziweze kuimarisha utoaji wa huduma za usambazaji wa umeme katika maeneo tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 65.79 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa*

i. Kuendelea na ujenzi wa laini kubwa ya umeme yenye uwezo wa kilovoti 132 pamoja na kufanya malipo kwa Mshauri Elekezi;
ii. Uwekaji wa mfumo wa kidigitali wa usimamizi na uendelezaji wa miundombinu ya umeme;
iii. Kuanza ujenzi wa miundombinu ya umeme wa jua pamoja vituo vya kupozea umeme katika maeneo ya Makunduchi, Ubago na Matemwe;
iv. Kusimamia masuala ya jinsia katika sekta ya nishati; na
v. Kuwajengea uwezo watendaji katika sekta ya nishati.

*Mradi wa Ulazaji wa Waya wa Umeme Baharini*

Mradi una lengo kuondoa changamaoto za umeme kwa ujenzi wa miundombinu ya nyaya za chini ya bahari. Mradi unatarajiwa kuweka waya mpya pamoja na ujenzi wa vituo vya kupokelea umeme katika maeneo ya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 16.72 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

*Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa*

- Kukamilisha taratibu za manunuzi ili kumpata Mshauri Elekezi na Mkandarasi wa utengenezaji wa nyaya za baharini, vifaa na usafirishaji wa umeme chini ya bahari.

*Mradi wa Uimarishaji wa Sekta ya Madini*

Mradi unalenga kuongeza ufanisi, usimamizi, maendeleo endelevu ya shughuli za uchimbaji na biashara ya madini. Mradi utasaidia kuboresha miundombinu, mazingira ya kazi, kuongeza mapato ya sekta ya madini, pamoja na kuimarisha mchango wa sekta hiyo katika ukuaji wa uchumi na ajira kwa wananchi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuboresha miundombinu na vifaa vya shughuli za madini;
ii. Kutoa mafunzo kwa wachimbaji na wadau wa sekta ya madini; na
iii. Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za uchimbaji.

## 5.16 Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu

Wizara ina lengo la kuharakisha mageuzi ya kidijitali kwa kusimamia maendeleo ya miundombinu ya TEHAMA na ubunifu. ili kuongeza ufanisi wa Serikali, kukuza uchumi wa kidijitali, kuimarisha usalama wa mifumo, taarifa na kuinua ustawi wa wananchi kwa ushindani wa Kitaifa na Kimataifa. Wizara hii inatekeleza miradi kupitia sekta kuu tatu ambazo ni Mawasiliano, Teknolojia ya Habari (TEHAMA) na Ubunifu. Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu moja ya maendeleo.

***Programu ya Mageuzi ya Kidigitali***

Programu ina lengo la kuimarisha mshikamano wa juhudi za Kitaifa katika kuendeleza mageuzi ya kidijitali kwa kuboresha huduma na miundombinu, kuimarisha mifumo na usalama wa taarifa, pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya sera na miongozo. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 41.37 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanzisha Mji wa Teknolojia, kuboresha na kuendeleza ujuzi wa kidijitali kwa wananchi, vijana na watumishi wa umma; na
ii. Kuanzisha Mfumo wa Serikali wa Kubadilishana Taarifa (Zanzibar Government Interoperability Platform- Zanxchange).

## 5.17 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

Wizara ina lengo la kusimamia fursa na vipaumbele vya uchumi unaotegemea rasilmali za baharini kwa ajili ya kuijenga Zanzibar mpya yenye uchumi wa kisasa. Aidha Wizara inazingatia kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu

ya bahari pamoja na kusimamia fursa za uwezeshaji na uwekezaji katika sekta ya uvuvi, mazao ya baharini, kilimo cha mwani, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu tatu (3) zitakazogharimu jumla ya TZS 193.24 bilioni (TZS 130.26 bilioni kutoka Serikalini na TZS 62.98 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu**

Programu hii inalenga kuendeleza sekta ya uvuvi wa bahari kuu kwa kutumia mbinu na teknolojia za kisasa, ili kuongeza mchango katika uchumi na kuboresha maisha ya wananchi. Kwa mwaka 2026/2027, programu inatarajia kutekeleza miradi minne (4) ya maendeleo.

***Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya Kusarifu na Kuchakata Samaki***

Mradi una lengo la kuimarisha sekta ya uvuvi katika kuongeza thamani bidhaa ya dagaa kwa kujenga viwanda vitakavyoshughulikia ukusanyaji, uhifadhi na usambazaji wa dagaa kwa masoko ya ndani na nje ya nchi ili kuongeza kipato na maendeleo endelevu kwa jamii. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 39.00 bilioni Kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanza ujenzi wa viwanda vya kuchakata Samaki Mkoani na Chamanangwe - Pemba; na
ii. Kuanza ujenzi wa kiwanda cha minofu ya samaki Fungurefu - Unguja.

***Mradi wa Uwanzishwaji wa Eneo Huru la Uwekezaji wa Uchumi wa Buluu***

Mradi una Lengo la kuimarisha uchumi wa Taifa kupitia rasilimali za bahari kwa kuanzisha eneo maalum la uwekezaji litakalovutia wawekezaji wa ndani na nje, kuongeza fursa za ajira na kuchochea maendeleo ya viwanda vinavyohusiana na uchumi wa buluu. Kwa mwaka wa 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 5.00 bilioni Kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Uwekaji wa miundombinu ya maji, umeme, barabara, mitaro na uzio kwa eneo la uwekezaji Fungurefu.

***Mradi wa Kukuza Usimamizi Endelevu wa Uvuvi na Ukuzaji wa Mazao ya Baharini Tanzania – TASFAM***

Mradi una lengo la kuimarisha usimamizi wa rasilimali za bahari na kuboresha upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa walengwa. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 45.41 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa madiko mawili (2) ya kisasa ya Samaki Kizimkazi na Wete;
ii. Ujenzi wa bandari ndogo ya uvuvi - Malindi;
iii. Ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mwani kwa maeneo ya Fungurefu, Pongwe, Tumbe, Chokocho na Kiuyu Mbuyuni;
iv. Uwekaji wa mitambo ya kuzalisha barafu na vyumba baridi katika maeneo ya Nungwi na Malindi - Unguja na Tumbe – Pemba;
v. Ujenzi wa chuo cha Uvuvi – Fungurefu Unguja;
vi. Ununuzi wa lori la kuhifadhia samaki;
vii. Ununuzi wa boti tisa (9) kwa ajili ya doria na utafiti; na
viii. Kufanya ukarabati wa Afisi katika majengo ya Nyangumi, Jodari na ZAFIRI.

***Mradi wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi***

Mradi una lengo la kuongeza tija endelevu, faida na biashara ya mbegu za mazao, uvuvi na ufugaji wa samaki, kwa kutilia mkazo uwezeshaji wa wanawake na ushiriki wa vijana. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 13.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ununuzi wa meli mbili (2) zenye mita 18m na 25m za uvuvi wa bahari kuu;

ii. Kuendelea kufanya utafiti wa uzalishaji na ukuzaji wa samaki wakiwemo majongoo bahari, kaa na mwatiko;
iii. Ujenzi wa vituo viwili vya mafunzo ya uvuvi na ufugaji wa viumbe bahari Unguja na Pemba;
iv. Ujenzi wa vituo vya kusarifu mwani na ununuzi wa vifaa vya maabara ya uzalishaji mbegu za mwani;
v. Ununuzi wa gari aina ya lori na jokofu la tani 10 kwa ajili ya Kampuni ya Uvuvi;
vi. Kufanya ukarabati wa makaushio manne (4) na chanja 80 zilizopo Kiuyu Mbuyuni - Pemba; na
vii. Kuanzisha mashamba darasa mawili ya ufugaji wa samaki kwa kutumia mabwawa na matangi; na
viii. Kuanzisha karakana kwa ajili ya matengenezo ya vifaa na mitambo - Unguja na Pemba.

**Programu ya Kuendeleza Wavuvi Wadogo Wadogo**

Lengo la Programu hii ni kuboresha uwezo wa wavuvi wadogo kwa kuwapatia rasilimali, ujuzi, na mazingira bora ya kufanya shughuli zao ili kuongeza ufanisi na uzalishaji katika shughuli zao. Kwa mwaka 2026/2027, programu inatarajia kutekeleza miradi minne (4) ya maendeleo.

***Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki***

Mradi una lengo la kuwawezesha wavuvi kwa kupata huduma bora na masoko ya uhakika, kwa kuwajengea miundombinu ya kisasa ya kuhifadhia na kuuzia samaki katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 24.04 bilioni Kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuendelea na ujenzi wa madiko na masoko ya samaki matano (5) katika maeneo ya Msuka, Kiwani na Kengeja kwa Pemba, Fukuchani na Pitanazako kwa Unguja; na

ii. Kuanza ujenzi wa madiko na masoko mapya kwa maeneo ya Kichuwani, Kojani na Mtambwe kwa Pemba, Unguja Ukuu, Kigomani, Tumbatu na Nungwi kwa Unguja.

***Mradi wa Uidhinishwaji wa Maabara ya ZAFIRI kwa Bidhaa za Uvuvi na Ufugaji wa Viumbe Maji na Kulipa Hadhi Zao la Mwani***

Mradi una lengo la kuimarisha ubora na ushindani wa bidhaa za uvuvi na ufugaji wa viumbe maji ili uweze kutoa huduma za upimaji na uthibitishaji wa viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa. Mradi pia unalenga kuimarisha uzalishaji wa zao la mwani kwa kuboresha miundombinu ya uhifadhi na uchakataji wa mwani, ili kuwawezesha wakulima kuongeza ubora wa mazao yao. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 16.21 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Uboreshaji wa miundombinu ya maabara pamoja na ununuzi wa vifaa;
ii. Ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba;
iii. Ujenzi wa kitalu cha utoaji mbegu bora na himilivu za mwani - Pemba.
iv. Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani - Unguja; na
v. Ujenzi wa vituo 10 vya kusarifu mwani Unguja na Pemba.

***Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini.***

Mradi una lengo la kuwawezesha wakulima wa mwani na wasindikaji wa mazao ya baharini kufikia maendeleo endelevu ya mnyororo wa thamani. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.11 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kuanzisha mashamba nane (8) ya majaribio ya ufugaji wa mwani na majongoo bahari;
ii. Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani na majongoo bahari – Chokocho Mkoani Pemba;

iii. Kutoa mafunzo kwa wanawake ambao ni wakulima wa mwani na majongoo bahari; na
iv. Kutoa mafunzo ya teknolojia ya kisasa ya kilimo cha mwani, kaa na majongoo bahari kwa wafanyakazi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

***Mradi wa Mashirikiano ya Kulinda na Kusimamia Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani***

Mradi una lengo la kuimarisha sekta ya uvuvi na usimamizi wa mazingira ili kuboresha usalama wa chakula, uhimilivu, pamoja na kuongeza ushiriki katika usimamizi wa matumizi ya rasilimali asilia kwa jamii za pwani. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 2.96 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya mafunzo kwa Maafisa Uvuvi wa Wilaya wanaohusika na usimamizi wa maeneo ya Hifadhi za Bahari;
ii. Uhamasishaji wa jamii juu ya uanzishwaji wa maeneo ya hifadhi kwa uvuvi wa pweza;
iii. Uandaaji wa mpango juu ya usimamizi wa ufungaji wa pweza unaozingatia eneo husika Kusini-Mashariki Pemba;
iv. Ununuzi wa mtambo baridi unaotumia nishati ya jua pamoja na kuwajengea uwezo juu ya uendeshaji wa mtambo;
v. Kuwajengea uwezo wavuvi juu ya mbinu bora za uhifadhi wa samaki baada ya mavuno;
vi. Ununuzi wa mashine za boti na zana za uvuvi kwa wavuvi wadogo wadogo unaozingatia uhifadhi wa mazingira;
vii. Kununua majokofu ya kuhifadhia samaki kwa wavuvi na wajasiriamali wa samaki;
viii. Kuwajengea uwezo wakulima wa mwani juu ya mbinu bora za ukulima wa mwani unaozingatia uhifaddi wa mazingira; na

ix. Ununuzi wa vifaa vya ukulima wa mwani kama chanja za kuanikia mwani pamoja na mashine za kutengenezea sabuni.

**Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia**

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu inayohusiana na uzalishaji, usambazaji na uhifadhi wa mafuta na gesi asilia ambayo itaongeza ufanisi katika mifumo ya usimamizi wa mafuta na gesi asilia itakayosaidia ukuaji wa uchumi. Kwa mwaka 2026/2027, programu inatarajia kutekeleza miradi miwili (2) ya maendeleo.

***Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia***

Mradi una lengo la kuimarisha usimamizi wa taarifa za mafuta na gesi asilia kupitia kituo cha Taifa cha kuhifadhi taarifa, ili kuhakikisha taarifa hizo zinatunzwa kwa usahihi na usalama. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 11.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuanza kwa ujenzi wa kituo cha kudumu cha kuhifadhia taarifa za mafuta na gesi asilia.

***Mradi wa Kufanya Utafiti wa Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa Njia ya Mtetemo 3D***

Mradi una lengo la kukusanya na kuchambua taarifa za utafutaji wa mafuta na gesi asilia kwa kutumia teknolojia ya mtetemo wa 3D ili kubaini kwa usahihi uwepo, ukubwa na muundo wa hifadhi za mafuta na gesi asilia. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 35.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kutoa uelewa na kushirikisha jamii juu ya suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta;
ii. Kufanya zoezi la uchukuaji, usafishaji na kutoa tafsiri za taarifa za mafuta na gesi asilia;
iii. Kusimamia ubora wa zoezi la uchukuaji wa taarifa; na
iv. Kufanya tathmni ya kimazingira (EIA).

## 5.18 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi

Wizara ina jukumu la kuendeleza miundombinu ya barabara kwa kupanga, kujenga, kukarabati na kudumisha mtandao wa barabara ili uwe salama, wa kudumu na wenye kukidhi viwango vya Kimataifa. Aidha, inasimamia ujenzi na matengenezo ya majengo ya umma pamoja na kuendeleza miundombinu ya usafiri wa anga na majini kupitia ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege, bandari na huduma za meli. Katika utekelezaji wa majukumu hayo, Wizara itaendelea na ujenzi wa barabara kuu, matengenezo na ukarabati wa barabara za mijini, pamoja na uwekaji wa taa za barabarani katika maeneo ya mijini na vijijini.

Kwa mwaka 2026/2027, Wizara inategemea kutekeleza programu saba (7) na miradi mitatu (3) yenye jumla ya TZS 1.79 trilioni, ambapo TZS 1.24 trilioni kutoka Serikali na TZS 557 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

### Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu

Programu ina lengo la kuunganisha miji mikuu ya Zanzibar kwa ujenzi wa barabara kuu zenye urefu km 159.5 – Unguja na Pemba kwa lengo la kurahisisha huduma za usafiri ili kukuza shughuli za kiuchumi, kijamii na uwekezaji. Barabara hizi ni kiunganishi cha miji na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo viwanja vya ndege na bandari. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 556.50 bilioni (TZS 342.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 214.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Ujenzi wa barabara ya Mwera – Dole – Mfenesini (km 14.3) na Dunga – Kilombero – Kinyasini (km 19.00);
ii. Ujenzi wa barabara ya Mkokotoni – Kinazini Junction - Nungwi (km 18.0), Mahonda – Donge – Mkokotoni (km 13.1), Mkwajuni – Matemwe (km7.0);
iii. Ujenzi wa barabara ya Tunguu – Dunga Jumba la Mawe (km 7.0), Mfenesini – Bumbwini (km 7.0);

iv. Ujenzi wa barabara ya Amani – Dunga (km 12.7), Jendele – Cheju – Kaebona – Unguja Ukuu (km7.0);
v. Ujenzi wa barabara ya Paje – Michamvi (km18.0);
vi. Ujenzi wa barabara ya Chake Chake – Wesha (km 7.4), Chwale – Kilindini – Konde Sokoni (km 24.4) na Kilindini – Micheweni (km5.2);
vii. Kufanya upembuzi yakinifu wa uanzishwaji wa reli ya Zanzibar;
viii. Kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa daraja la Charawe – Chwaka;
ix. Kuandaa Mpango Mkuu wa Usafiri Tanzania (JICA); na
x. Ujenzi wa mitaro/misingi ya kuondolea maji ya mvua (Storm Water) katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Zanzibar.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Chake Chake – Wete (km 22.1); na
ii. Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tunguu – Makunduchi (km 48), Mkoani – Chake Chake (km 43.5) na Fumba – Kisauni (km 12).

**Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani**

Programu itahusisha ujenzi wa barabara za ndani na vijijini zenye urefu wa km 144.71 pamoja na km 46.2 zinazoingia katika maeneo ya Hoteli za Kitalii Unguja na Pemba. Programu itaunganisha mitaa na maeneo mengine ikiwemo barabara kuu. Aidha, kukamilika kwa programu hii kutasaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuongeza haiba ya kupendezesha miji na mitaa. Kwa mwaka 2026/2027, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 151.72 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa barabara ya Chanjamjawiri – Tundauwa (km 12), Macho Mane – Wawi – Vitongoji (km 5.0), Mizingani – Wambaa – Sisumizini – Fundu Lagoon (km 8.0), Mtambile – Kengeja – Mwambe (km 5.0);
ii. Ujenzi wa barabara ya Kwakozi – Mwera Pongwe (km 1.64), Kwakibunju – Maungani – Kisakasaka (km 3.59), Maungani Vijijini – Shakani (km

5.9) Shakani – Nyamanzi (km 1.2), Jumbi – Ipa (km 1.2), Bavuai camp – Migombani JWTZ (km 3.75);

iii. Ujenzi wa barabara zinaingia katika maeneo mbali mbali ikiwemo kambi ya JKU Kama (km 0.95), Ziwani Police (km 2.67), Mitondooni Bakery, (km 1.79), Kisauni Mtundani (km 1.57), Kisauni Msikiti/Kanisa (km 1.71), Mwera (km 1.31), Vituo vya Michezo vya Wilaya (km 5);

iv. Ujenzi wa barabara ya Mtambile – Kangaani (km 3.4), Jadida – Bugujiko – Mtemani (km 2), Kuyuni – Kalani – Zawadini (km 1.54);

v. Ujenzi wa barabara ya Kizimbani – Popo (km 1.5), Kwale – Kidemeni Pemba (km 1.0), Machui/Dole – Kizimbani (km 8), Kiboje – Uchukuni (km 3.8);

vi. Ujenzi wa barabara za kuingia hoteli ya Michamvi (km 18), Muyuni – Nungwi (km13.3);

vii. Ujenzi wa barabara za kuunganisha hoteli (Chwaka – Uroa – Pongwe – Matemwe – Muyuni pamoja na Makunduchi – Paje – Bwejuu – Michamvi km 15); na

viii. Ujenzi wa barabara nyenginezo za jamii na hoteli (Unguja na Pemba, km 50).

***Mradi wa Ujenzi wa Barabara Zinazoingia katika Mji wa Michezo Fumba***

Mradi unalenga kurahisisha upatikanaji wa huduma, kuongeza fursa za uwekezaji, pamoja na kuimarisha hadhi ya eneo hilo kama sehemu muhimu ya maendeleo ya kisasa Zanzibar. Kwa mwaka 2026/2027 mradi umepangiwa jumla ya TZS 269.08 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa barabara ya Mazizini (ZRA) – Fumba (km 19.9); na

ii. Ujenzi wa barabara za ndani zinazoingia katika Mji wa Michezo wa Fumba.

**Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini**

Programu inalenga kuimarisha haiba ya mji wa Zanzibar kwa ujenzi wa barabara katika maeneo ya mjini. Programu inahusu ujenzi wa km 54.93 za barabara za mjini na uimarishaji wa barabara katika maeneo ya mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa mwaka 2026/2027, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 95.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa barabara ya Maruhubi – Karakana – Mtopepo (km 1.4), Mtoni – Bububu (km 4.2), barabara ya Karume (Kariakoo – Mkunazini na Mlandege - Maisara – Bwawani km 3.0);
ii. Ujenzi wa barabara ya Fuoni – Kombeni – Kisauni – Fumba (km 25);
iii. Ujenzi wa barabara zinazozunguka ziwa Maboga (km 11);
iv. Ujenzi wa barabara ya Kariakoo – Magomeni – Mwanakwerekwe (km 2.7), Kariakoo (km 2.73), Amani – Biziredi (km 2.5); na
v. Ujenzi wa madaraja matatu (3) ya watembea kwa miguu.

**Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)**

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ambayo itashajihisha ukuaji wa uchumi katika visiwa vya Zanzibar. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 162.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Ujenzi wa bwawa la Mwantenga na Ziwa Maboga; na
ii. Ujenzi wa barabara ya Mnazi Mmoja – Malindi (Creek Road) na Malawi Road (km 2.4).

**Programu ya Utunzaji na Matengenezo wa Barabara**

Programu ina lengo la kuboresha usalama barabarani, kurahisisha usafiri, kupunguza gharama za uzalishaji na kuvutia uwekezaji sambamba na kushughulikia changamoto za uchakavu, mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la matumizi ya barabara. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 45.20 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kukarabati na kuboresha barabara zilizochakaa; na
ii. Kuimarisha mifumo ya maji ili kukabiliana na athari za tabianchi.

**Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege.**

Programu ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kufikia viwango vya Kimataifa na kuwa na uwezo wa kupokea ndege aina ya "Code 4C". Aidha, programu inalenga kuongeza idadi ya wasafiri hususan watalii wanaoingia Zanzibar. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 210.50 bilioni, ambapo TZS 70.50 bilioni ni kutoka Serikali na TZS 140.00 bilioni ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali.***

i. Ujenzi wa jengo la kuongozea ndege (Control tower);
ii. Ujenzi wa maegesho ya mdege (Apron);
iii. Usimamizi wa mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege Pemba; na
iv. Ujenzi wa jengo la abiria Terminal II AAKIA.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

- Ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba.

***Programu ya Kuimarisha Bandari***

Programu inalenga kuimarisha miundombinu ya bandari ili kuongeza ufanisi wa huduma za usafirishaji na biashara ya baharini nchini. Utekelezaji wa programu unatarajiwa kuongeza uwezo wa bandari kuhudumia mizigo na meli kwa ufanisi zaidi, kuimarisha usalama wa huduma za bandari, na kupunguza gharama za usafirishaji na matengenezo ya meli. Aidha, maendeleo hayo yataiwezesha Zanzibar kuwa kitovu cha shughuli za usafirishaji wa mizigo kwa kupitishia katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepangiwa jumla ya TZS 265.50 bilioni (TZS 225.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 40.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

i. Ujenzi wa bandari jumuishi ya Mangapwani; na
ii. Ujenzi wa barabara zinazoingia maeneo ya bandari ya Mangapwani.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

- Ujenzi wa bandari ya abiria na mizigo ya Mpigaduri - Maruhubi.

***Mradi wa Uwekaji wa Taa kwa Barabara za Mjini na Vijijini***

Mradi una lengo la kuboresha usalama na ufanisi wa matumizi ya barabara kwa kuweka mifumo ya kisasa ya taa katika maeneo ya mjini na vijijini. Kupitia utekelezaji wake, mradi utapunguza ajali na vitendo vya uhalifu, kurahisisha shughuli za kiuchumi nyakati za usiku, na kuongeza ubora wa maisha kwa wananchi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 8.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Uwekaji wa taa za barabarani.

***Mradi wa Ujenzi wa Mitaro/Misingi ya Kuondoa Maji ya Mvua katika Maeneo ya Mji wa Zanzibar***

Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya maji machafu na ukusanyaji wa maji ya mvua ili kusaidia kupunguza athari za mafuriko wakati wa mvua kubwa. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuboresha mazingira ya makazi na shughuli za kijamii na kiuchumi kwa kupunguza uharibifu wa barabara, nyumba na miundombinu mingine. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 30.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kujenga mitaro ya maji ya mvua;
ii. Kujenga mabwawa ya kutunzia maji ya mvua; na
iii. Kujenga mitaro katika barabara zinazoendelea kujengwa.

## 5.19 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

Wizara ina jukumu la kusimamia sekta ya utalii na mambo ya kale kwa kuibua na kuendeleza vivutio vipya vya utalii pamoja na kuendelea kuitangaza sekta kuwa kivutio kikuu cha utalii duniani. Aidha, Wizara imepanga kuimarisha uhifadhi wa urithi wa kihistoria, kiutamaduni, kuboresha miundombinu ya maeneo ya utalii, kuongeza ubunifu wa bidhaa za utalii zenye tija pamoja na kuendeleza kampeni za Kimataifa za kuitangaza Zanzibar katika masoko mapya ya watalii. Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza programu mbili na mradi mmoja wa maendeleo kwa jumla ya TZS 57.53 bilioni (TZS 42.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 15.03 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria**

Programu ina lengo la kuendeleza Sekta ya Utalii kwa kulinda, kuhifadhi na kutunza maeneo ya kihistoria yaliopo nchini kwa faida ya kizazi cha sasa na baadae. Vile vile, programu inasimamia kukuza shughuli za utalii kwa kuongeza fursa za ajira, vivutio vya utalii na kuongeza pato la Taifa. Kwa mwaka 2026/2027, programu imepanga kutekeleza miradi mitatu (3) yenye jumla ya TZS 45.53 bilioni (TZS 30.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 15.03 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Mradi wa Ukarabati wa Makumbusho na Maeneo ya Kihistoria***

Mradi una lengo la kuimarisha uhifadhi, mvuto na ubora wa huduma katika maeneo ya urithi wa Zanzibar. Mradi huu utaongeza thamani ya utalii wa kihistoria ili kuchochea mapato na ajira. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa jumla ya TZS 15.50 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Usanifu na uboreshaji wa makumbusho na maeneo ya kihistoria;
ii. Kuimarisha makumbusho na maeneo ya kihistoria Mnazi Mmoja na Amani - Unguja;
iii. Kuyafanyia matengenezo maeneo ya kihistoria ya Kichokochwe, Fufuni, Jambangome, Ole Mandani, Chwaka Tumbe na Mkamandume Pujini kwa

Pemba, Mvuleni, Msikiti wa Kizimkazi, Pango la Kuumbi, Dunga, Bi-Khole - Bungi, Mnazi Mmoja, Makumbusho ya bahari, Bustani ya Victoria, Makumbusho ya Sanaa ya Kisasa kwa Unguja; na

iv. Kuweka uzio katika maeneo ya kihistoria.

***Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Mji Mkongwe***

Mradi una lengo la kulinda maisha ya wakaazi na wageni kwa kupunguza hatari ya kuanguka kwa majengo chakavu, kuimarisha usalama wa makaazi na mazingira ya kuishi. Mradi utachangia kuboresha ustawi wa jamii, kulinda urithi wa Mji Mkongwe na kuimarisha mazingira salama na endelevu ya makaazi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuendelea na ukarabati wa nyumba 15 hatarishi katika eneo la Mji Mkongwe.

***Mradi wa Kukamilisha Ukarabati wa Jengo la Beit Al Jaib***

Mradi unalenga kurejesha alama muhimu ya kihistoria katika urithi wa Mji Mkongwe, pamoja na kuimarisha na kuongeza mvuto wa Mji Mkongwe kwa watalii. Aidha, hatua hii inalenga kuanzisha na kuimarisha mashirikiano ya kimkakati baina ya Zanzibar na Oman katika usimamizi na uendelezaji wa pamoja wa hazina hii ya kihistoria. Kwa mwaka 2026/2027, mradi huu umepangiwa jumla ya 15.03 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuendelea na ukarabati wa jengo la Beit Al Jaib.

**Programu ya Kuendeleza na Kuimarisha Vivutio vya Utalii**

Programu ina lengo la kuimarisha na kuongeza ubora wa vivutio vya utalii ili kuvutia wageni na kuongeza ushindani. Programu itajumuisha uendelezaji wa miundombinu, uhifadhi wa rasilimali za asili na kihistoria pamoja na kuboresha huduma za utalii kwa lengo la kuongeza mapato na ajira. Kwa mwaka 2026/2027,

programu imepanga kugharimu jumla ya TZS 11.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kuendeleza na kuimarisha vivutio kumi (10) vya utalii katika maeneo mbalimbali ikiwemo Nyanjali (Mangapwani), Mkokotoni, Kajengwa, Uzi, Kilimani Muungoni kwa Unguja na Vitongoji, Gando, Pango Samaki – Muambe, Kisiwa Ndege – Tumbe, Pembeni – Ziwani na Popo Kidike kwa Pemba.

***Mradi wa Ugatuzi na Uendeshaji wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar ZITOD***

Mradi huu unalenga kuimarisha hadhi, uwezo na utendaji wa chuo husika ili kukiwezesha kutambulika rasmi kama Kituo cha Umahiri katika utoaji wa mafunzo ya utalii na ukarimu. Kupitia mradi huu, chuo kitaimarishwa katika maeneo ya miundombinu ya mafunzo, rasilimali watu, mitaala inayokidhi viwango vya Kimataifa, pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya kujifunzia. Aidha, mradi unalenga kukifanya chuo kutambulika Kikanda na Kimataifa kama Taasisi bora ya mafunzo ya utalii na ukarimu kupitia ushirikiano na vyuo na taasisi za kimataifa, uimarishaji wa viwango vya ubora pamoja na kupata ithibati kutoka taasisi zinazotambulika Kimataifa. Kwa mwaka 2026/2027, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa***

i. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya Chuo ikiwemo majengo yanayotoa huduma mbalimbali za mafunzo na vitendo (majiko, sehemu za kufulia nguo na madarasa); na
ii. Ununuzi wa vifaa vya mafunzo, kuimarisha mazingira ya kujifunzia, miundombinu ya usafi na usalama.

### 5.20 Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji

Wizara imeanzishwa kwa lengo la kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kukuza ujuzi wa kisasa katika masuala ya ujasiriamali, biashara, ubunifu na matumizi ya teknolojia pamoja na kuongeza fursa za ajira zenye tija. Aidha, Wizara inalenga kuimarisha ushiriki wa vijana katika maendeleo ya Taifa kwa kuwawezesha kushiriki katika shughuli za uzalishaji, uwekezaji, kilimo, uvuvi, viwanda vidogo, uchumi wa buluu na huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi ili kuongeza kipato chao na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana.

Kwa mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza mradi mmoja (1) utakaogharimu jumla ya TZS 10.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Mradi wa Vituo vya Mafunzo Kwa Vijana Awamu ya Pili***

Mradi una lengo la kuwajengea uwezo vijana kwa kuwapatia mafunzo ya stadi za maisha na ufundi. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 10.00 bilioni kutoka Serikalini.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Ujenzi wa vituo viwili (2) vya uwezeshaji wananchi kiuchumi na vijana Unguja na Pemba.

#### 5.20.1 Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar

Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar ni taasisi iliyoanzishwa kwa lengo la kuratibu, kuimarisha na kusimamia juhudi za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ili kuongeza ushiriki wao katika shughuli za uzalishaji na biashara, kupunguza umaskini na kuongeza ajira kwa vijana, wanawake na makundi maalum. Taasisi hii hutekeleza majukumu ya kuandaa na kusimamia programu za uwezeshaji kiuchumi, kutoa elimu ya ujasiriamali na stadi za kazi, kuratibu upatikanaji wa mikopo na mitaji midogo, kuwezesha vikundi vya kijamii na vyama vya ushirika, kufuatilia na kutathmini miradi ya kiuchumi pamoja na kukuza biashara ndogo ndogo na za kati (SMEs) kupitia ushirikiano

kati ya Serikali na wadau wa maendeleo kwa lengo la kuwawezesha wananchi kujitegemea kiuchumi.

Kwa mwaka 2026/2027, Taasisi imepanga kutekeleza miradi miwili (2) itakayogharimu TZS 47.30 bilioni (TZS 37.20 bilioni kutoka Serikalini na TZS 10.10 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo na Wakati***

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wakati kwa kuwapatia mikopo itakayowasaidia kuongeza mitaji yao ili waweze kujitegemea. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Abudhabi kupitia Mfuko wa Khalifa (Khalifa Fund). Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 42.30 bilioni (TZS 37.20 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.10 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

***Shughuli Iliopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali***

- Kutoa mikopo kwa wajasiriamali, wazalishaji wadogo na wakati.

***Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo***

i. Kutoa mikopo kwa wafanyabiashara, wazalishaji na wajasiriamali wadogo na wakati; na
ii. Kuratibu na kusimamia utoaji na urejeshwaji wa mikopo.

***Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja)***

Mradi una lengo la kukuza fursa za kiuchumi kwa wanawake pamoja na kuwezesha vikundi vya kijamii kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kukuza masoko ya bidhaa. Kwa mwaka 2026/2027, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 5.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Shughuli Iliyopangwa Kutekelezwa***

- Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali, wazalishaji na wafanyabiashara.

## 6.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI

Kwa mwaka 2026/2027, Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar imepanga kusimamia na kufuatilia pamoja na kufanya Tathmini ya Mpango wa Maendeleo kama ifuatavyo:

i. Kuandaa na kuchapisha Mapitio ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya 2021-2026;
ii. Kutoa uwelewa kwa Wizara, Idara, Taasisi zinazojitegemea, Serikali za Mitaa, Taasisi Binafsi, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na Asasi za Kiraia juu ya matumizi ya Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Zanzibar ya mwaka 2026;
iii. Kuandaa na kuchapisha ripoti ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo (ZADEP 2021-2026);
iv. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo iliyokamilika na inayoendelea;
v. Kufanya ufuatiliaji na tathmini juu ya utendaji wa Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Wizara, Taasisi na Serikali za Mitaa na kuvijengea uwezo ili viweze kufanya majukumu yao ipasavyo;
vi. Kuandaa Mkakati wa Mawasiliano wa kupata taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na Kuimarisha mfumo wa ZiPS;
vii. Kuandaa na kuchapisha Ripoti ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa Zanzibar kwa mwaka 2026–2027; na
viii. Kuandaa na kuchapisha ripoti ya Hiari ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (Voluntary Local Review) kwa ngazi ya Mikoa kwa mwaka 2026/2027.

## 7.0 WASHIRIKA WA MAENDELEO

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027, Washirika wa Maendeleo watakaochangia bajeti ya programu na miradi ya maendeleo ni pamoja na: ADAPTATION FUND (AF), AfDB, ALSF, AUSTRIA, BADEA, SHEIKH ZAID CHARITABLE FOUNDATION - ABUUDHABI UAE, LAD, EDF EU, EDCF, KOREA, EXIM BANK OF KOREA, GEF/UNDP, WORLDBANK/

KOREA/UNCDF, ENABEL, EU, UNDP/FAO, FCDO, WORLD BANK/ IMF/AfDB/EU, PHARM ACCESS INTERNATIONAL, UNICREDIT BANK (AUSTRIA), GERMAN/GIZ, GERMAN-KfW, KFW, DLI-GPE/ SIDA, UNICREDIT BANK (AUSTRIA), GLOBAL FUND, INDIA –EXIM BANK, UNDP/IRISH EMBASSY, JICA, KOICA, WORLD BANK/NORWAY, BADEA/SAUDI FUNDS/KUWAIT FUNDS, KOREAN GOVERNMENT, GIZ/KFW, BIG WIN PHILANTHROPY UK, AMREF, NETHERLAND, NORWAY, NORAD, IFAD/ OPEC, IFAD, GATE FOUNDATION, SAUDI FUNDS, STBF, SULTANATE OF OMAN, UAE, NEMC, UKEF – CITI BANK, UKEF - DEUTCH BANK, UNDP, UNFPA, UNICEF, GAVI, UN-WOMEN, na WORLD BANK (IDA).

## 8.0 HITIMISHO

Kitabu hiki cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2026 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2026/2027 kimeandaliwa kwa ushirikiano wa karibu kati ya Serikali, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia pamoja na wananchi kwa lengo la kuweka msingi madhubuti wa utekelezaji wa vipaumbele vya maendeleo ya Taifa. Ushirikiano huo umechangia kuandaliwa kwa Mpango unaolenga kuongeza tija katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo na kuimarisha ustawi wa wananchi.

Katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango huu, Serikali itaendelea kuelekeza nguvu katika kukuza uchumi, kuimarisha huduma za jamii, kuongeza fursa za ajira na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Utekelezaji wa programu na miradi iliyopangwa unatarajiwa kuwa nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 pamoja na Mipango mingine ya maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Kwa upande mwingine, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zinapaswa kuhakikisha kuwa maeneo yote ya vipaumbele yaliyoainishwa katika Kitabu hiki yanatekelezwa kwa ufanisi kwa kuzingatia mipango na bajeti zilizopangwa. Aidha, Tume ya Mipango itaendelea kuratibu utekelezaji wa programu na miradi

ya maendeleo pamoja na usimamizi wa mtiririko wa fedha ili kuhakikisha utekelezaji wa shughuli hizo unafanyika kwa wakati na kuzingatia malengo yaliyowekwa.

Sambamba na hilo, Taasisi zote za Serikali zinatakiwa kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwa kuwasilisha taarifa sahihi za utekelezaji wa shughuli za maendeleo kila robo mwaka kwa Tume ya Mipango. Taarifa hizo zitasaidia kupima kiwango cha utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa pamoja na kuhakikisha matumizi bora na yenye tija ya rasilimali za umma na misaada ya Washirika wa Maendeleo.

Mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026/2027 yatategemea ushirikiano, uwajibikaji na mshikamano wa wadau wote katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kuijenga Zanzibar yenye uchumi imara, maendeleo endelevu na maisha bora kwa wananchi wake.

Kurasa zinazofuata zinaonesha viambatisho vya mgawanyo wa fedha za programu na miradi ya maendeleo kwa Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali kwa mwaka 2026/2027 ikijumuisha fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo.

# Kiambatisho namba 1: PROGRAMU NA MIRADI INAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA FEDHA ZA SERIKALI NA WASHIRIKA WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2026/2027 (TZS MILIONI)

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| **1** | **OFISI YA RAIS - IKULU** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Uimarishaji wa Majengo ya Ikulu | 6,000,000 | 7,000,000 | | | | 7,000,000 |
| | ii) Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mhe. Rais | 2,000,000 | | | | | - |
| | iii) Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano ya Mfumo wa Rais | 700,000 | | | | | - |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **8,700,000** | **7,000,000** | | **-** | **-** | **7,000,000** |
| **5** | **OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** | | | | | | |
| | **Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma (Phase II)** | 1,000,000 | | | | | - |
| | **Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria** | 500,000 | | | | | - |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Kusaidia Kukabiliana na Kesi za Ukatili kwa Utoaji wa Huduma ya Haki ya Masuala ya Kijinsia kwa Wanawake | | | UN-WOMEN | 147,501 | | 147,501 |
| | ii) Upatikanaji wa Haki za Kisheria | | | UNDP/ IRISH EMBASSY | 1,717,577 | | 1,717,577 |
| | ii) Kujenga Msingi Imara wa Mapambano Dhidi ya Rushwa Tanzania (BSAAT) | | | Foreign Commonwealth and Development Office (FCDO) | 3,184,802 | | 3,184,802 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **1,500,000** | **-** | | **5,049,879** | **-** | **5,049,879** |
| **26** | **MAHKAMA KUU** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Mikoa | 13,000,000 | | | | | - |
| | ii) Mradi wa Uboreshaji wa Mahkama | 600,000 | 1,600,000 | WORLD BANK | | 35,002,572 | 36,602,572 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **13,600,000** | **1,600,000** | | **-** | **35,002,572** | **36,602,572** |
| **4** | **AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Kijeshi cha Kisasa cha Idara Maalum za SMZ | | 70,000,000 | | | | 70,000,000 |
| | ii) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Idara Maalum za SMZ | | 30,000,000 | | | | 30,000,000 |
| | iii) Mradi wa Ujenzi wa Masoko | | 65,000,000 | | | | 65,000,000 |
| | vi) Mradi wa Zanzibar Salama | 25,750,000 | 40,176,619 | | | | 40,176,619 |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | v) Mradi wa Kuimarisha Haki Jinai Chuo cha | 18,000,000 | 40,000,000 | | | | 40,000,000 |
| | vi) Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri Soko la Mwanakwerekwe | 20,000,000 | 47,000,000 | | | | 47,000,000 |
| | vii) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi wa Masheha | 8,000,000 | 40,000,000 | | | | 40,000,000 |
| | viii) Mradi wa Kijani na Kuimarisha Miji Sasa | | | EU | 2,212,343 | | 2,212,343 |
| | ix) Mradi wa Mji bila Taka | 10,000,000 | - | | | | - |
| | x) Mradi wa Usafi na Upendezeshaji wa Miji | | 18,000,000 | | | | 18,000,000 |
| | xi) Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Ngazi ya Jamii | | | WORLD BANK/KOREA | | 5,643,544 | 5,643,544 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **81,750,000** | **350,176,619** | | **2,212,343** | **5,643,544** | **358,032,505** |
| **41** | **WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili | 1,500,000 | 2,364,712 | VITAL STRATEGIES | 257,249 | | 2,621,961 |
| | ii) Kuimarisha Miundombinu ya Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 2,000,000 | 1,635,288 | | | | 1,635,288 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **3,500,000** | **4,000,000** | | **257,249** | **-** | **4,257,249** |
| **44** | **KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM | 2,500,000 | | | | | - |
| | ii) Mradi wa Kuimarisha Shughuli za Uzamiaji na Uokozi | 2,500,000 | 12,784,000 | | | | 12,784,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **5,000,000** | **12,784,000** | | **-** | **-** | **12,784,000** |
| **46** | **KIKOSI CHA VALANTIA** | | | | | | |
| | Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Mahanga ya KVZ | 5,524,000 | 6,400,000 | | | | 6,400,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **5,524,000** | **6,400,000** | | **-** | **-** | **6,400,000** |
| **43** | **CHUO CHA MAFUNZO** | | | | | | |
| | Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga - Chuo Cha Mafunzo | 3,578,000 | 3,400,000 | | | | 3,400,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **3,578,000** | **3,400,000** | | **-** | **-** | **3,400,000** |
| **42** | **JESHI LA KUJENGA UCHUMI** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi waNyumba na Mahanga ya Kambi za JKU | 5,986,000 | | | | | - |
| | ii) Mradi wa Ujenzi wa Dakhalia | 3,125,100 | 8,523,281 | | | | 8,523,281 |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | iii) Uimarishaji wa Utoaji wa Huduma za Wakala wa Ulinzi JKU | 5,423,000 | 4,240,000 | | | | 4,240,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **14,534,100** | **12,763,281** | | **-** | **-** | **12,763,281** |
| **45** | **KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari - KZU | 3,000,000 | 4,000,000 | | | | 4,000,000 |
| | ii) Mradi wa Ununuzi wa Magari ya Zimamoto | 2,550,000 | | AUSTRIA | | 3,558,991 | 3,558,991 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **5,550,000** | **4,000,000** | | **-** | **3,558,991** | **7,558,991** |
| **2** | **OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS** | | | | | | |
| | i) Mradi wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira | 4,500,000 | 5,000,000 | | | | 5,000,000 |
| | ii) Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Jamii ya Pwani | | | AF (UNDP) | 1,407,837 | | 1,407,837 |
| | iii) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Kitaifa na Kuziwezesha Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi | | | BENKI YA DUNIA | 551,781 | | 551,781 |
| | iv) Mradi Shirikishi wa Kuhimili Mifumo ya Ikolojia ya Bahari na Ukanda wa Pwani na Shughuli za Kujipatia Kipato | | | UNEP | 153,785 | | 153,785 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **4,500,000** | **5,000,000** | | **2,113,403** | **-** | **7,113,403** |
| **34** | **MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Kuirithisha Zanzibar Kijani | 1,000,000 | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | ii) Mfumo wa Kitaifa wa Taarifa za Usimamizi wa Mazingira (EIMS) | | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |
| | iii) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Kitaifa na Kuziwezesha Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi | | | BENKI YA DUNIA | 111,977 | | 111,977 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **1,000,000** | **2,500,000** | | **111,977** | **-** | **2,611,977** |
| **32** | **MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA MADAWA YA KULEVYA** | | | | | | |
| | Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya | 4,500,000 | 8,250,000 | | | | 8,250,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **4,500,000** | **8,250,000** | | **-** | **-** | **8,250,000** |
| **3** | **OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS - SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI** | | | | | | |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | **Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III)** | 100,000 | | BENKI YA DUNIA | | 40,000,000 | 40,000,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Nyumba za Makamu wa Pili wa Rais | 2,000,000 | | | | | - |
| | ii) Ukarabati wa Ofisi ya Uratibu Dar es Salaam | 550,000 | | | | | - |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **2,650,000** | **-** | | **-** | **40,000,000** | **40,000,000** |
| **8** | **WIZARA YA AFYA** | | | | | | |
| | **Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar** | 1,000,000 | 1,000,000 | USAID/GF | 7,692,136 | | 8,692,136 |
| | **Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto** | 1,000,000 | 1,000,000 | GAVI/STBF/ UNFPA/ USAID-JHPIEGO | 4,323,216 | | 5,323,216 |
| | **Programu ya Kudhibiti Maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma** | 1,000,000 | 1,000,000 | GF | 4,632,798 | | 5,632,798 |
| | **Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya** | 35,350,000 | | | | | - |
| | i) Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja | | 20,906,292 | | | | 20,906,292 |
| | ii) Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa Kusini Unguja, Kusini Pemba na Kaskazini Pemba | | 3,300,000 | Sheikh Zaid Charitable Foundation - ABBUDHABI UAE | 12,862,458 | | 16,162,458 |
| | iii) Ujenzi wa Maabara ya ZFDA Pemba | | 4,200,000 | | | | 4,200,000 |
| | iv) Ujenzi Kituo cha Usimamizi na Udhibiti wa Maradhi ya Mripuko (ZPHI) | | 6,400,000 | | | | 6,400,000 |
| | **Programu ya Kuimarisha huduma za Mama na Mtoto** | | | WORLD BANK | | 23,395,241 | 23,395,241 |
| | **Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi** | 20,000,000 | 40,050,000 | | | | 40,050,000 |
| | **Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa** | 3,000,000 | | | | | - |
| | **Programu ya Jamii ni Afya** | 2,000,000 | 2,000,000 | | 1,000,000 | | 3,000,000 |
| | **Programu ya Kusaidia Watu Wasiojiweza Kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya** | 1,000,000 | | | | | - |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | **Programu ya Kuimarisha Nguvu Kazi** | 2,000,000 | 2,000,000 | | | | 2,000,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Kuimarisha Mifumo ya Kidigitali | 1,000,000 | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | ii) Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja | 14,400,000 | 15,700,000 | BADEA/SAUDI FUNDS/ KUWAIT FUNDS | | 45,193,266 | 60,893,266 |
| | iii) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia - Bunguni | 1,700,000 | 1,966,500 | ECDF KOREA (EXIM BANK) | | 4,139,139 | 6,105,639 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **83,450,000** | **100,522,792** | | **30,510,607** | **72,727,646** | **203,761,044** |
| **25** | **HOSPITALI YA MNAZI MMOJA** | | | | | | |
| | Mradi wa Ununuzi wa Vifaa Tiba | 2,000,000 | 3,000,000 | | | | 3,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **2,000,000** | **3,000,000** | | - | - | **3,000,000** |
| **14** | **WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI** | | | | | | |
| | **Programu ya Ujenzi wa Nyumba na Uimarishaji wa Mji** | 300,120,000 | 300,920,000 | | | | 300,920,000 |
| | **Programu ya Upangaji wa Miji na Usimamizi wa Ardhi** | 35,565,000 | | | | | - |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **335,685,000** | **300,920,000** | | - | - | **300,920,000** |
| **17** | **WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuendeleza Viwanda** | | | | | | |
| | i) Kuanzisha na kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks) | 35,560,000 | 25,742,000 | | | | 25,742,000 |
| | **Programu ya Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar** | 10,803,870 | 8,520,000 | | | | 8,520,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **46,363,870** | **34,262,000** | | - | - | **34,262,000** |
| **11** | **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI** | | | | | | |
| | **Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu** | 247,647,900 | 355,177,760 | AfDB/WB/UK/UAE/ BADEA/SIDA-GPE/ UNICEF/AUSTRIA | 84,673,925 | 158,554,913 | 598,406,598 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Kuimarisha Upatikanaji wa Vifaa vya Kujifunzi na Kufundishia | 39,208,100 | 65,897,743 | BADEA/ UNICREDIT BANK (AUSTRIA) | 280,500 | 1,482,913 | 67,661,156 |
| | ii) Uimarishaji wa Elimu ya Juu | 35,000,000 | 45,000,000 | | | | 45,000,000 |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **321,856,000** | **466,075,503** | | **84,954,425** | **160,037,826** | **711,067,754** |
| 9 | **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO** | | | | | | |
| | **Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali** | | | | | | |
| | i) Ukamilishaji wa Ofisi za Serikali | 59,576,410 | 111,886,646 | | | | 111,886,646 |
| | ii) Ujenzi wa Mji wa Serikali | 66,722,160 | 55,078,000 | | | | 55,078,000 |
| | **Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)** | | | BENKI YA DUNIA | | 32,000,000 | 32,000,000 |
| | **Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP)** | 350,000 | 700,000 | NORWAY | | 2,541,000 | 3,241,000 |
| | **Programu ya Ulipaji wa Fidia za Miradi ya Maendeleo** | 210,399,750 | 170,399,750 | | | | 170,399,750 |
| | **Programu ya Kusaidia Watu Wasiojiweza Kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar** | | | PHARM ACCESS INTERNATIONAL | 350,000 | | 350,000 |
| | **Mradi** | | | | | | |
| | i) Msaada wa Kiufundi kwa ajili ya Kukuza Uwezo wa Uhamasishaji Utafutaji Rasilimali Fedha | | | WORLD BANK /UNCDF /BADEA /GERMANY/GIZ | 4,770,945 | | 4,770,945 |
| | ii) Ulipaji wa Madeni kwa Miradi ya Maendeleo | 312,000,000 | 600,000,000 | | | | 600,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **649,048,320** | **938,064,396** | | **5,120,945** | **34,541,000** | **977,726,341** |
| 24 | **TUME YA MIPANGO** | | | | | | |
| | **Programu ya Uratibu wa Mikakati ya Ukuaji Jumuishi** | 4,500,000 | 9,500,000 | | | | 9,500,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Uratibu na Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo | 5,500,000 | 14,900,000 | | | | 14,900,000 |
| | ii) Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo Kitaifa, Kikanda na Kimataifa | 1,800,000 | 2,420,000 | | | | 2,420,000 |
| | iii) Kuendeleza Tafiti za Kimkakati | 1,000,000 | 2,200,000 | | | | 2,200,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **12,800,000** | **29,020,000** | | - | - | **29,020,000** |
| 23 | **OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI** | | | | | | |
| | i) Mpango Mkuu wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) | | | WB | | 6,402,232 | 6,402,232 |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | ii) Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia | 2,000,000 | 1,864,618 | UN-WOMEN | 250,000 | | 2,114,618 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **2,000,000** | **1,864,618** | | **250,000** | **6,402,232** | **8,516,850** |
| **22** | **OFISI YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI** | | | | | | |
| | Mradi wa Utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IPSAS ACCRUAL) | 1,023,875 | | | | | - |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **1,023,875** | - | | - | - | - |
| **56** | **WIZARA YA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya | 40,550,000 | 18,029,760 | | | | 18,029,760 |
| | ii) Ujenzi wa Kiwanja Kipya cha Michezo | 372,900,000 | 186,872,560 | | | | 186,872,560 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni | 3,000,000 | | | | | - |
| | ii) Ujenzi wa Kijiji cha Utamaduni na Kituo cha Ubunifu wa Kazi za Sanaa | | 15,000,000 | | | | 15,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **416,450,000** | **219,902,320** | - | - | - | **219,902,320** |
| **6** | **WIZARA YA KAZI NA UWEKEZAJI** | | | | | | |
| | **Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji** | 15,000,000 | 15,000,000 | | | | 15,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **15,000,000** | **15,000,000** | | - | - | **15,000,000** |
| **12** | **WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO** | | | | | | |
| | **Programu ya Maendeleo ya Mifugo** | | | | | | |
| | i) Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu | 2,500,000 | 2,500,000 | | | | 2,500,000 |
| | ii) Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa Wafugaji Wadogo Unaozingatia Mabadiliko ya Tabianchi (C-SDTP) | | | IFAD/OPEC | | 7,800,000 | 7,800,000 |
| | iii) Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa Kuongeza Tija na Uzalishaji Kupitia Huduma za Kisasa za Kilimo katika Umwagiliaji | 200,000 | | KOREAN GOVERNMENT (KRC) | 3,473,750 | | 3,473,750 |
| | **Programu ya Maendeleo ya Tafiti za Kilimo na Mifugo** | | | | | | |
| | i) Kuimarisha Shamba la Viungo na Bustani ya Mimea | | 5,550,000 | | | | 5,550,000 |
| | ii) Kuimarisha Miundombinu na Uwezo wa Utafiti wa Kilimo, Maliasili na Mifugo | | 3,000,000 | | | | 3,000,000 |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | **Programu ya Maendeleo ya Kilimo** | | | | | | |
| | i) Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula | 20,000,000 | 75,500,000 | | | | 75,500,000 |
| | ii) Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (TFSRP) | | | WB | 6,500,000 | 33,213,525 | 39,713,525 |
| | iii) Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejeshaji wa Ardhi (FOLUR) | | | GEF/WWF | 841,730 | | 841,730 |
| | iv) Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa Kukuza Uchumi Jumuishi | | | EDF EU | 4,631,750 | | 4,631,750 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Kuanzisha Bustani ya Mimea (Botanic Garden) | 2,000,000 | | | | | - |
| | ii) Ulinzi wa Misitu ya Mwambao wa Zanzibar kwa Manufaa Mchanganyiko | | | GEF/UNDP | 1,995,225 | | 1,995,225 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **24,700,000** | **86,550,000** | | **17,442,455** | **41,013,525** | **145,005,980** |
| **19** | **WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,WAZEE NA WATOTO** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Hifadhi ya Wazee | 1,500,000 | 3,500,000 | | | | 3,500,000 |
| | ii) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Kulelea Watoto Yatima | | 3,500,000 | | | | 3,500,000 |
| | iii) Mradi wa Kutokomeza Udhalilishaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana | | | EU/ UN WOMEN | 636,321 | | 636,321 |
| | iv) Mradi Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja) | | | WORLD BANK | 255,000 | 9,003,720 | 9,258,720 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **1,500,000** | **7,000,000** | | **891,321** | **9,003,720** | **16,895,041** |
| **15** | **WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI** | | | | | | |
| | **Program ya Kuimarisha Mifumo ya Maji Zanzibar** | | | | | | |
| | i) Uimarishaji wa Huduma za Maji kwa Mikoa ya Unguja | | 35,550,000 | | | | 35,550,000 |
| | ii) Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar | 2,516,670 | | INDIA (EXIM BANK) | | 13,893,762 | 13,893,762 |
| | iii) Kuimarisha Usalama wa Maji Zanzibar | 2,600,000 | | GIZ/KFW | 9,614,085 | | 9,614,085 |
| | iv) Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi (ZUWDFIP) | 1,541,000 | | JICA | | 25,000,000 | 25,000,000 |
| | v) Usimamizi na Uangalizi Bora wa Maji | | | UNICEF | 30,000 | | 30,000 |
| | vi) Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar | 15,776,890 | | | | | - |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | vii) Uboreshaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Kaskazini Unguja | 2,600,000 | | | | | - |
| | viii) Kuandaa Mpango Mkuu wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zanzibar | | | GERMANY/KfW | 840,738 | | 840,738 |
| | ix) Kuimarisha Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira (Awamu ya II) | | | WB | 2,500,000 | | 2,500,000 |
| | xi) Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji kwa Skimu Tisa (9) | | 50,200,000 | | | | 50,200,000 |
| | xii) Ujenzi wa Matangi Kumi (10) | | 5,125,000 | | | | 5,125,000 |
| | xiii) Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji Maji Safi katika Mji wa Michezo - Fumba | | 19,205,900 | | | | 19,205,900 |
| | xiv) Uwekaji wa Mifumo ya Usafirishaji wa Maji Taka katika Mji wa Michezo - Fumba | | 6,285,388 | | | | 6,285,388 |
| | **Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar** | | | | | | |
| | i) Maboresho ya Mfumo wa Usambazaji na Usafirishaji wa Umeme Zanzibar | | 41,722,257 | | | | 41,722,257 |
| | ii) Kuanzisha Kinu cha Kufua Umeme kwa Kutumia Majenereta | | 59,621,560 | | | | 59,621,560 |
| | iii) Ujenzi wa Kituo Kipya cha Kupozea Umeme | | 20,475,000 | | | | 20,475,000 |
| | iv) Uwekaji wa Miundombinu ya Kuhifadhia na Kusafirishia Umeme | | 32,155,798 | | | | 32,155,798 |
| | v) Uwekaji wa Miundombinu ya Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Nishati ya Jua katika Visima vya | | 12,580,500 | | | | 12,580,500 |
| | vi) Kuimarisha Miundombinu na Uzalishaji wa Umeme | | 31,000,000 | | | | 31,000,000 |
| | vii) Kuimarisha Miundombinu ya Umeme | 7,000,000 | | | | | - |
| | viii) Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati | | | BENKI YA DUNIA | | 65,793,927 | 65,793,927 |
| | ix) Uboreshaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar | 33,355,685 | | | | | - |
| | x) Ulazaji wa Waya wa Umeme Baharini | | | AfDB | | 16,721,195 | 16,721,195 |
| | xi) Udhibiti, Ugavi na Matumizi Endelevu ya Nishati ya Umeme Zanzibar | | | NORWAY/ NORAD | 9,003,720 | | 9,003,720 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Uimarishaji wa Sekta ya Madini | | 1,500,000 | | | | 1,500,000 |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **65,390,245** | **315,421,403** | | **21,988,544** | **121,408,883** | **458,818,830** |
| **59** | **WIZARA YA MAWASILIANO , TEKNOLOJIA YA HABARI NA UBUNIFU** | | | | | | |
| | **Programu ya Mageuzi ya Kidigitali** | | | | | | |
| | i) Kulaza Mkonga wa Kimataifa wa Baharini Zanzibar (International Gateway) | 30,000,900 | | | | | - |
| | ii) Utoaji wa Huduma ya Mtandao katika Maeneo ya Umma (Public Wi-Fi ) | 10,050,000 | | | | | - |
| | iii) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Data | 30,000,000 | | | | | - |
| | iv) Uimarishaji Mfumo wa Mawasiliano | 6,000,000 | | | | | - |
| | v) Uanzishwaji wa Mji wa Teknolojia | | 31,365,000 | | | | 31,365,000 |
| | vi) Mfumo wa Serikali wa Kubadilishana Taarifa (Zanxchange) | | 10,000,000 | | | | 10,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **76,050,900** | **41,365,000** | **-** | **-** | **-** | **41,365,000** |
| **13** | **WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI** | | | | | | |
| | **Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR) | 7,000,000 | 11,000,000 | | | | 11,000,000 |
| | ii) Usambazaji wa Gesi | 9,000,000 | | | | | |
| | iii) Kufanya Utafiti wa Utafutaji wa Mafuta kwa Njia ya Mtetemo ya 3D | | 35,000,000 | | | | 35,000,000 |
| | **Programu ya Kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Shumba | 29,994,810 | | | | | |
| | ii) Ujenzi wa Viwanda vya Kusarifu na Kuchakata Samaki | 51,000,000 | 39,000,000 | | | | 39,000,000 |
| | iii) Uwanzishwaji wa Eneo Huru la Uwekezaji wa Uchumi wa Buluu - Fungurefu | | 5,000,000 | | | | 5,000,000 |
| | iv) Kukuza Usimamizi Endelevu wa Uvuvi na Ukuzaji wa Viumbe Maji wa Bahari Tanzania - TASFAM | | | WB (IDA) | | 45,412,300 | 45,412,300 |
| | v) Kuendeleza Uvuvi na Kilimo (AFDP) | | | IFAD | | 13,498,655 | 13,498,655 |
| | **Programu ya Kuendeleza Wavuvi Wadogo Wadogo** | | | | | | |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | i) Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki | 27,675,560 | 24,044,040 | | | | 24,044,040 |
| | ii) Uidhinishwaji wa Maabara ya ZAFIRI kwa Bidhaa za Uvuvi na Ufugaji wa Viumbe Maji na Kulipa Hadhi zao la Mwani | | 16,211,351 | | | | 16,211,351 |
| | iii) Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Mwani (SESEP) | 6,575,000 | | | | | - |
| | iv) Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini | | | KOICA | 1,118,000 | | 1,118,000 |
| | v) Mashirikiano ya Kulinda na Kusimamia Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani | | | UNDP/FAO | 2,958,365 | | 2,958,365 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **131,245,370** | **130,255,391** | | **4,076,365** | **58,910,955** | **193,242,711** |
| 61 | **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI** | | | | | | |
| | **Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu** | 133,392,956 | 340,000,000 | BADEA/SF/ UKEF/ DEUTCH BANK /EXIM BANK OF CHINA | | 214,500,000 | 554,500,000 |
| | **Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani** | 78,034,000 | 151,721,361 | | | | 151,721,361 |
| | **Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini** | 35,000,000 | 95,000,000 | | | | 95,000,000 |
| | **Programu ya Ujenzi wa Barabara zinazoingia katika Mji wa Michezo Fumba** | | 269,079,843 | | | | 269,079,843 |
| | **Programu ya Utunzaji na Matengenezo wa Barabara** | | 45,200,000 | | | | 45,200,000 |
| | **Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)** | | | BENKI YA DUNIA | | 162,500,000 | 162,500,000 |
| | **Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba | 2,000,000 | 4,500,000 | UKEF/CITI BANK | | 140,000,000 | 144,500,000 |
| | ii) Ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II AAKIA | 30,000,000 | | | | | - |
| | iii) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II AAKIA (Phase II) | 30,000,000 | 30,000,000 | | | | 30,000,000 |
| | iv) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi | 22,500,000 | | | | | - |
| | v) Ujenzi wa Apron katika kiwanja cha Ndege cha AAKIA | 40,000,000 | 36,000,000 | | | | 36,000,000 |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | **Programu ya Kuimarisha Bandari** | | | | | | |
| | i) Ujenzi wa Bandari Jumuishi - Mangapwani | 205,100,364 | 225,500,000 | | | | 225,500,000 |
| | ii) Ujenzi wa Bandari ya Abiria Maruhubi | | | NETHERLAND | 40,000,000 | | 40,000,000 |
| | **Miradi** | | | | | | |
| | i) Uwekaji wa Kamera za Kusimamia Usafiri Barabarani | 1,873,000 | | | | | - |
| | ii) Uwekaji wa Taa kwa Barabara ambazo hazina Taa za Barabarani Mjini na Vijijini | | 8,000,000 | | | | 8,000,000 |
| | iii) Upembuzi Yakinifu wa Uanzishwaji wa Reli Zanzibar na Mpango Mkuu wa Usafiri Tanzania (JICA) | | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | iv) Upembuzi Yakinifu wa Daraja la Charawe - Chwaka | | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | v) Ujenzi wa Mitaro/Misingi ya Kuondolea Maji ya Mvua (Storm Water) katika maeneo Mbali Mbali ya Mji wa Zanzibar | 270,000,000 | 30,000,000 | | | | 30,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **847,900,320** | **1,237,001,204** | | **40,000,000** | **517,000,000** | **1,794,001,204** |
| **10** | **WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE** | | | | | | |
| | **Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria** | | | | | | |
| | i) Ukarabati wa Makumbusho na Maeneo ya Kihistoria | 6,000,000 | 15,500,000 | | | | 15,500,000 |
| | ii) Ukarabati wa Majengo ya Mji Mkongwe | 10,000,000 | 15,000,000 | | | | 15,000,000 |
| | iii) Ukarabati wa Jengo la Beit Al Ajaib | | | SULTANATE OF OMAN | 15,025,822 | | 15,025,822 |
| | **Programu ya Kuendeleza na Kuimarisha Vivutio vya Utalii** | 6,000,000 | 11,000,000 | | | | 11,000,000 |
| | **Mradi** | | | | | | |
| | Ugatuzi na Uendeshaji wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar (ZITOD) | | 1,000,000 | | | | 1,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **22,000,000** | **42,500,000** | | **15,025,822** | - | **57,525,822** |
| **55** | **WIZARA YA VIJANA, AJIRA NA UWEZESHAJI** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Maendeleo ya Vijana | 16,500,000 | 10,000,000 | | | | 10,000,000 |

| FUNGU | PROGRAMU/MIRADI | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2025/2026 | MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2026/2027 | MICHANGO YA WAHISANI ("000") | | | JUMLA YA BAJETI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | MUHISANI | RUZUKU | MKOPO | |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **16,500,000** | **10,000,000** | | **-** | **-** | **10,000,000** |
| **105** | **WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** | | | | | | |
| | i) Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa | 4,500,000 | 37,200,000 | UAE | 5,100,000 | | 42,300,000 |
| | ii) Mradi Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja) | | | WORLD BANK | 5,000,000 | | 5,000,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **4,500,000** | **37,200,000** | | **10,100,000** | **-** | **47,300,000** |
| | **JUMLA YA KUBWA** | **3,231,350,000** | **4,433,798,527** | | **240,105,336** | **1,105,250,893** | **5,779,154,755** |
| | **JUMLA YA FEDHA ZA WAHISANI** | | | | | **1,345,356,229** | |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YA MAENDELEO** | | | | | | **5,779,154,755** |